# Nipashe

Jumatatu Aprili 25, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0580926

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




SportPesa

CHEZA USHINDE SASA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Mwalimu** Nyerere alikataa kuwekewa damu ya mzungu

UKURASA 3



# ARV zilizokwisha muda zagundulika

• **CAG** apendekeza ziteketezwe pamoja na vifaa vya upasuaji Muhimbili, MSD... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**ASAKWA TUHUMA ZA MAUAJI KISHA KUFUKIA MWILI KWENYE SHIMO**

JESHI la Polisi mkoani hapa, linamtafuta mkulima wa Kijiji cha Barikiwa, Wilaya...

UKURASA WA 4

**KINANA AJITISHWA KERO ZA WAFANYABIASHARA**

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, amewataka...

UKURASA WA 7

**CCM YAWAONYA VIONGOZI WANAOSUMBUA BODABODA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewaonya viongozi wanaosababisha...




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene (kulia), Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (wapili kulia) na Ofisa Mkuu wa Mkaguzi wa Ndani, Benedicto Baragomwa (kushoto) wakielekea katika futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wabunge, mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. **Habari Uk. 4. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Gwajima acharuka watoto kufanyiana ukatili shuleni

UKURASA 3



## Mbunge afariki dunia akijifungua

UKURASA 2

**MICHEZO** DODOMA JIJI YATAMBA KUANZA LIGI UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza wakati alipofungua Maonesho ya Miaka 58 ya Muungano kwenye viwanja vya Maisara , Zanzibar jana. Kulia ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mbunge afariki dunia akijifungua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM) Mkoa wa Rukwa, Irene Ndyamkama, amefariki dunia jana katika Hospitali ya Tumbi mkoani Pwani alikokuwa akipatiwa matibabu, huku ikidaiwa alikuwa akijifungua kwa oparesheni.

Spika wa Bunge, Dk.Tulia Ackson, alithibitisha kutokea kwa kifo hicho na kutoa pole kwa familia na wananchi wa Mkoa huo.

"Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama natoa pole kwa familia ya marehemu ndugu, jamaa, waheshimiwa wabunge na wananchi wa Mkoa wa Rukwa, Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira katika kipindi hiki kigumu,"alisema.

Aidha, alisema Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na familia ya marehemu inaratibu mipango ya mazishi na taarifa zaidi zitaendelea kutolewa.

Pamoja na Ofisi ya Bunge kutoeleza chanzo cha kifo chake, lakini taarifa kutoka kwa watu wa karibu zinaeleza alifariki wakati akijifungua kwa upasuaji, na kwamba mtoto alipona na yupo chini ya uangalizi maalum.

**WABUNGE WAMWELEZEA**

Akimzungumzia marehemu, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Jacqline Kainja, alisema: "Irene alikuwa ni binti mpambanaji sana asiyekubali kushindwa na mwenye msimamo sana na pia alikuwa mcheshi sana ukikaa naye lazima ucheke."

"Muda mwingi nikikaa lazima anashauri namna ya kupambana ndoto na kutokubali kushindwa hadi kuhakikisha umekuwa mshindi," alisema.

Kwa upande wake, Mbunge wa viti maalum (CCM), Juliana Shonza, katika ukurasa wake wa Instagram aliandika kuwa "Ni vigumu kuamini kama hauko nasi Mheshimiwa Irene jana tulikuwa wote bungeni kwenye semina pole sana Mheshimiwa Anna Lupembe kwa kumpoteza binti yako mpendwa."

Naye, Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alisema akiwa Mbunge anayetokea Mkoa wa Rukwa msiba huo wameupokea katika hali ya maumivu makali kwa kuwa alikuwa anacheka na kila mtu.

"Alikuwa anacheka na kila mtu, hata kama kuna jambo lakini lazima awe kwenye sura ya furaha Irene ni mwanamke ambaye alikuwa anapambana sana alikuwa haamini katika kushindwa, alikuwa ni mtu ambaye alikuwa akitamani kujifunza na kila alicho nacho alitamani 'kushare' na wenzake alikuwa anaamini alichonacho huyu hakijui anaweza kumsaidia kujifunza."

"Hakuwa mchoyo wa kile ambacho aidha amejifunza au anakijua kumpatia na mtu mwingine kukijua, huyo ndo Irene ambaye naweza kumzungumzia simfahamu sana lakini namfahamu tangu akiwa Chadema aligombea ubunge wa viti maalum uchaguzi wa mwaka 2015 katika Mkoa wa Katavi kupitia Chadema na alishika nafasi ya kwanza kumuacha Rhoda Kunchela,"alisema.

Alisema alimfahamu wakati huo na hata maamuzi yalipofanyika hakuwa mtu wa kusema sema au kulalamika.

"Na kwa huu muda ambao alikuwa amehamia CCM na kugombea ubunge wa viti maalum alikuwa anakuja jimboni kwangu, ni mtu ambaye kwa kweli alikuwa anatoa ushirikiano kwa sisi wabunge wa majimbo Mkoa wa Rukwa,"alisema.

Alisema Rukwa imepoteza mtu muhimu mwenye umri mdogo ambaye alikuwa na uwezo ambao Mungu amemjalia.

Mbunge wa Mpanda Mjini (CCM), Sebastiani Kapufi, alisema marehemu alikuwa akimuita Mjomba kutokana na kuwa mwanafamilia.

"Mama yake ni Mbunge mwenzangu Wilaya yetu moja ya Mpanda, Mungu wetu wa mbinguni kweli ameweka kifo katika usiri mkubwa ili tusimkufuru yeye Mwenyezi Mungu aliye mweza wa yote."

"Hivyo mapenzi yake yatimizwe na mja wake ampumzishe mahali pema peponi ili nasi tunaoishi katika ulimwengu huu uliojaa mafumbo tuweze kukatana nae kesho mbinguni, apumzike kwa amani,"alisema.

Mbunge wa Kilindi, Omary Kigua, alisema ni Mbunge kijana na alikuwa anasifa ya ucheshi kwa wabunge wote.

Mbunge wa Kasulu Vijijini (CCM), Augustino Vuma alisema bunge limepata msiba mzito ambapo Irene alikuwa Mbunge kijana, mcheshi na rafiki wa watu wengi na alikuwa anapigania maendeleo ya Mkoa wa Rukwa.

Alisema wabunge watamkumbuka sana kutokana na kuwapigania wanawake.

**CCM YAMLILIA**

Katika hatua nyingine, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa za kifo cha Mbunge huyo.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema Mwenyekiti wa CCM na Rais Samia Suluhu Hassan amesema chama kimepoteza mwanachama na kiongozi muhimu aliyekuwa na mchango mkubwa kwa CCM na utumishi wa umma husussani wanawake wa Mkoa wa Rukwa.

"Tumepoteza mwanachama wa CCM na kiongozi ambaye mchango wake katika utumishi wa umma hautosahaulika, alikuwa ni kiongozi mahiri na aliyependa kujitolea kwa shughuli za maendeleo husussani ya wanawake na watoto hakuchoka nyakati zote.

Ndugu Samia Suluhu Hassan Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,"alisema.

Alieleza kuwa Mbunge huyo ametumikia nafasi mbalimbali ambapo hadi Mauti yanamfika alikuwa Mbunge wa Viti Maalum anayewakilisha Wanawake kwa tiketi ya CCM kutoka Mkoa wa Rukwa.

Baadhi ya maswali yaliyoulizwa na mbunge huyo ni pamoja na kutaka kujua mpango wa serikali wa kuendeleza zao la miwa kwa wananchi wa wilaya ya Kalambo, na lini serikali itakarabati meli ya Mv. Liemba pamoja na kujenga meli mpya zitakazochochea ukuaji wa uchumi wa mkoa wa Rukwa.

# ARV zilizokwisha muda zagundulika

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini kuwapo dawa zenye thamani ya Sh. bilioni 23.04 zilizokwisha muda wake katika maghala ya Bohari Kuu ya Dawa (MSD) na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

CAG Charles Kichere anabainisha hayo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2020/2 iliyowasilishwa bungeni jijini hapa Aprili 12, mwaka huu, hivyo kuwa wazi kwa umma.

Anafafanua kuwa kiwango cha kwisha muda wa dawa kwa mwaka wa fedha 2020/21 kilikuwa asilimia tano ya gharama za mauzo ya Sh. bilioni 196.83 sawa na kiwango kilichoripotiwa mwaka 2019/20 cha asilimia tano.

"Kiwango hiki kimezidi kiwango kinachotakiwa kwa asilimia mbili kama kilivyoelezwa katika Aya ya 7.3.3 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za MSD wa mwezi Juni 2018.

"Uchambuzi wangu pia ulibaini kuwa MSD ilikuwa na jumla ya bidhaa 7,676,436 za thamani ya Sh. bilioni 22.8 zilizopitwa na muda ambazo zilikuwa kwenye maghala ya MSD kuanzia tarehe 16 Aprili 2000 hadi 30 Juni 2021.

"Aidha, nilibaini MSD ilipokea fedha kutoka kwa wafadhili ambazo ni dola za Marekani 239,023.92 ili kugharamia kuharibu dawa za kupunguza makali ya VVU/UKIMWI. Hata hivyo, ingawa ruhusa ya kuteketeza dawa hizo ilishatolewa na Wizara ya Fedha na Mipango tangu tarehe 7 Oktoba 2021, dawa hizo hazikuharibiwa hadi wakati wa ukaguzi mwezi Desemba 2021.

"Pia, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili nilibaini kuwapo kwa ucheleweshaji wa kuomba vibali vya uhakiki wa vifaatiba vya kuanzia mwaka 2014 hadi Juni 2020, ambavyo ni dawa, vifaa vya matumizi ya upasuaji na vitendanishi vilivopitwa na muda kutoka katika mamlaka za serikali zinazohusika.

"Vifaatiba hivi vilivyopitwa na wakati/visivyotumika vilikuwa vya thamani ya Sh. milioni 235. Maombi ya vibali yalitumwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali tarehe 29 Septemba 2020 na 22 Septemba 2020," anabainisha.

CAG anaendelea kufafanua kuwa hali hiyo ni kinyume cha Aya ya 26 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma (Toleo Lililorekebishwa la Mwaka 2019) inayotaka maombi kuwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ndani ya siku 21 za kazi baada ya hasara kutokea.

Anasema MSD na MNH zinaingia kwenye gharama zisizo za lazima za uhifadhi na ulinzi wa bidhaa kwenye maghala ambazo hazitumiki, pia kuendelea kuwapo kwa dawa zilizoisha muda wake kunahatarisha afya za watumishi wanaofanya kazi kwenye maghala hayo.

"Ninapendekeza MSD iteketeze dawa zilizoisha muda ambazo kibali chake kimetolewa na ishirikiane na MNH kufuatilia vibali vya kuteketeza dawa na vifaa tiba ambavyo vimepitwa na muda," CAG anawasilisha hoja yake.

# Mwalimu Nyerere alikataa kuwekewa damu ya mzungu

**Na Jenifer Gilla**

ALIYEKUWA Katibu Muhtasi wa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Anna Mwansasu, amesema kuwa Mwalimu Julius Nyerere katika hali ya utani alisema kuwa akiwekewa damu ya mzungu hatokuwa yeye tena.

Aliyasema hayo juzi katika hafla ya kumbukizi ya miaka 100 ya kuzaliwa Hayati Mwalimu Nyerere, iliyoandaliwa na Mama Maria Nyerere, nyumbani kwake Msasani Dar es Salaam, akikumbushia jinsi kiongozi huyo alivyopenda kutaniana na wafanyakazi wake.

"Mimi wakati huo nilikuwa Geneva, kwenye ofisi yake ya Tume ya Kusini, kabla ya kifo chake nilipata bahati ya kwenda London kumuona. Nilipofika niliweza kuonana naye.

"Mwalimu aliniambia, Anna naumwa, wameniambia itabidi niongezewe damu, lakini wakiniongezea damu si itakuwa ya 'mzungu'. Sasa wakiniwekea damu ya mzungu si nitakuwa sio Kambarage tena," alisema Anna huku watu wakiangua vicheko.

Alisema kuwa licha ya kuwa kwenye maumivu makali wakati akiwa hospitalini hapo, Mwalimu aliongea kwa utani ili kuwatia moyo wa matumaini na kuwafurahisha waliokwenda kumuangalia hali inayoonyesha upendo na ukarimu aliokuwa nao kwa waliomzunguka.

Anna aliongeza kuwa, Hayati Mwalimu Nyerere alikuwa pia ni mtu mwenye utu na alipenda kusaidia kwa haraka watu wa aina yeyote.

"Tuliofanya kazi na Mwalimu huwa tunaulizwa, Je mwalimu alikuwa ni mtu wa namna gani? Jibu ni Mwalimu alikuwa na utu sana, ubinadamu aliokuwa nao ulifanya awe mwema sana kwa wafanyakazi. Shida ya mfanyakazi yeyote ikimfikia hakusita kusaidia," alisema.

Vilevile, alisema kuwa Mwalimu alikuwa anachukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa watu wanaomzunguka ikiwamo wafanyakazi wake hawamuogopi ikiwamo kutaniana na kucheka nao.

"Mwalimu alikuwa akitaniana na kucheka na wafanyakazi wa ngazi za chini kuliko wale wa ngazi za juu,aliokuwa akishughulika nao kwenye mambo makubwa yaliyohusu uongozi wa taifa letu," alisema.

Vile vile, alisema Mwalimu Nyerere aliwaheshimu na kuwapenda wafanyakazi wanawake na alipotaka kuwasiliana nao alipenda kutanguliza neno mama yangu au mama zangu.

Anna alimshukuru Mama Maria Nyerere kwa kuwakumbuka na kuwapa mwaliko huo wa kwenda kuadhimisha pamoja naye kumbukumbu hiyo.

"Hongera sana Mama Maria kwa kuolewa na Julius Nyerere alikuwa kiongozi mahiri sana Tanzania na maarufu sana barani Afrika na duniani. Mwalimu alituasa Uhuru ni Kazi na sasa tunasema 'Kazi Iendelee'," alisema.

# Gwajima aja juu watoto kufanyiana ukatili shuleni

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, ameeleza kusikitishwa na tabia ya baadhi ya wanafunzi kufanyiana ukatili mashuleni.

Gwajima alizungumzia matukio hayo juzi mkoani Shinyanga, wakati akipokea taarifa ya uzinduzi wa Programu ya malezi na makuzi bora ya mtoto kwa njia ya mtandao, kutoka Shirika la ICS ambalo linajihusisha na shughuli za utetezi wa haki za watoto na wanawake mkoani humo.

Alisema sasa hivi kumekithiri mmomonyoko wa maadili kwa sababu ya wazazi kuwa na shughuli nyingi za maisha na kusahau malezi ya watoto wao, hivyo kusababisha kuanza kufanyiana ukatili wenyewe hasa maeneo ya shule.

"Nimekuwa nikipokea meseji nyingi sana kuhusu watoto kufanyiana ukatili wao wenyewe mashuleni, wakienda huko msalani wanafanyiana vitu vya ajabu," alisema Waziri Gwajima.

"Naagiza maofisa ustawi wa jamii toeni elimu mashuleni kwa kushirikiana na walimu ya kupinga ukatili kwa sababu tumezoea kusikia watu wazima wakiwafanyia ukatili watoto, lakini sasa hivi wameanza kufanyiana ukatili wao wenyewe sijui tunaelekea wapi" alihoji.

Aidha, ameipongeza ICS kwa kuanzisha programu hiyo ya malezi na makuzi bora ya mtoto kwa njia ya mtandao, ambayo ana imani itasaidia wazazi kufundisha watoto wao



pamoja na kupunguza matukio ya ukatili.

Naye Mkuu wa wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema Programu hiyo ambayo inatumika kwenye simu janja, itapunguza pia ubize wa wazazi kuchati vitu visivyo vya maana, bali watakuwa wakisoma mafundisho mbalimbali na kulea watoto wao katika maadili mema.

Mkurugenzi wa Shirika la ICS, Kudely Sokoine, alisema wameanzisha programu hiyo ili kufikia wazazi wengi, ambao watakuwa wakijifunza mara kwa mara na kuboresha malezi ya watoto wao.

Alisema katika programu hiyo kuna vipindi 12, ambavyo mzazi atakuwa akisoma kwa wiki kipindi kimoja, na malengo yao ni kufikia wazazi 6,000 lakini kwa sasa wameanza na wazazi 1,100.


# NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **HOLYNESS & RESPISHERS COMPANY LIMITED, MOPEH COMPANY LIMITED** na **JADA INVESTMENT LIMITED** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD,** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | HOLLYNESS & RESPISHERS COMPANY LIMITED | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | Suzana Samwel Ganjiro | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Sokoine Uyole-Mbeya |
| 2 | Ratifa J Pelamio | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Masawe Ilemi-Mbeya |
| 3 | Zuena J Mwanyanje | Nyumba mbili zenye mkataba wa mauziano | Ndola Mbalizi-Mbeya |
| 4 | | | NKUYU NSALALA-MBEYA |
| 5 | Mansour Athuman Mbarouk | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Ulambya-Mbeya |
| 6 | Anyisisye Mwasimali | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mbalizi-Mbeya |
| 7 | Sauli Galus Ndelwa | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mwakibete-Mbeya |
| 8 | Elias Ally Sanga | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Hasanga-Mbeya |
| 9 | Asina Stephano Litimba | Nyumba yenye leseni cha makazi | Itongo, Mwakibete-Mbeya |
| 10 | Burton W Chombe | Nyumba yenye hati miliki kiwanja No.219, Kitalu D | Mbalizi-Mbeya |
| | MOPEH COMPANY LIMITED - NOTISI/TANGAZO LA MNADA WA MARUDIO | | |
| 11 | Thomas M Mayalla | Nyumba Namba Yenye Hati Miliki Kiwanja No.149 Kitalu E Eneo La Majengo Kahama | Majengo-Kahama |
| 12 | Khamisi A. Assad | Nyumba Yenye Hati Miliki Kiwanja No 13 Kitalu A,Eneo La Isaka Kahama Na Kiwanja Chenye Hati Miliki No.11, Kitalu A, Eneo la Isaka Yenye Jina La Rehema Soud Hilali | Isaka- Kahama |
| | JADA INVESTMENT LIMITED PROFESSIONAL COLLECTOR | | |
| 13 | Abdallah S Kombo | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Ubungo Msewe-Dar es salaam |
| 14 | Kaaro General Traders Ltd | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Golani-Dar es salaam |
| 15 | Heri B Rashid | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mzinga-Dar es salaam |
| 16 | Niku A Kapyela | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Vikindu- Dar es salaam |
| 17 | Irene V Lusasi | Kiwanja Chenye Mkataba Wa Mauziano | Vikindu- Dar es Salaam |
| 18 | Anita F Ngaiza | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano, Ambayo Haija Kamilika | Virobo, Chanika-Dar es Salaam |
| 19 | Kassim S Lipolilwe | Kiwanja Chenye Mkataba Wa Mauziano | Kongowe Mlaleni- Dar es Salaam |
| 20 | Abdulkadir J Miliki | Kiwanja Chenye Mkataba Wa Mauziano | Kisemvumle-Dar es Salaam |
| 21 | Mekijiti O Mwinduchi | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano | Mombasa, Moshi Bar- Dar es Salaam |
| 22 | Khatibu O Jihada | Kiwanja Chenye Mkataba Wa Mauziano | Tambani-Mkuranga-Dar es Salaam |
| 23 | Peter N Nyawaya | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano Iliyopo Kitunda | Kitunda-Dar es Salaam |
| 24 | Tito Anthony Magarya | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano Iliyopo Kivule | Kivule-Dar es Salaam |
| 25 | Alvera George Mushi | Kiwanja Chenye Mkataba Mauziano Kilichopo Chanika Na Kiwanja Chenye Leseni Ya Makazi Kilichopo Moshi Bar Gongo La Mboto | Chanika na Moshi Bar Gongo La Mboto-Der es Salaam |
| 26 | Richard Kijimyabupi Buluba | Kiwanja Chenye Mkataba Wa Mauziano Kilichopo | Kigobedi Mkuranga-Dar es Salaam |
| 27 | Henry Joseph Mallya | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano Iliyopo Kibamba | Kibamba -Dar es Salaam |
| 28 | George Salumu Alli | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano | Chamazi -Dar es Salaam |
| 29 | Evody Hendry Shayo | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano Iliyopo | Temeke Mashine ya Maji- Dar es Salaam |
| 30 | Hamis Mohamed Nyanda | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano Iliyopo Gongo La Mboto | Gongo Lamboto-Dar es Salaam |
| 31 | David Nyamuhanga Gimonge | Kiwanja Chenye Mkataba Wa Mauziano Kilichopo Magore Na Kiwanja Chenye Hati Miliki Kiwanja No., Kitalu Kilichopo Kigamboni | Magore, Kigamboni-Dar es Salaam |
| 32 | Mabula O Sweya | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano Iliyopo Mtaa Wa Nyerubi Chanika Na Nyumba Yenye Leseni Ya Makazi Iliyopo Nzasa Charambe | Nyerubi Chanika na Nzasa Charambe-Dar es Salaam |
| 33 | Rehema Michael Sapali | Nyumba Yenye Mkataba Wa Mauziano | Toangoma-Dar es Salaam |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (Transfer of ownership, na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Hollyness & Respishers Company Limited**
**S.L.P 714**
**Bukoba**
**Namba za simu: 0762058614**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji.**
**Mopeh Company Limited**
**S.L.P 519 Dar es Salaam**
**Namba za Simu; 0713639979/0673335528**

**NA**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Jada Investment Limited**
**S.L.P 4110**
**Dar es Salaam**
**NAMBA ZA SIMU: 0788493699**

**Na**

**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Namba za simu: 0768790399, 0754774949**

216822402



Mkuu wa Wilaya ya Tanga. Hashimu Mgandilwa, akizungumza na wageni waalikwa waliohudhuria hafla ya futari iliyoandaliwa na Benki ya Exim Tanzania kwa ajili ya wateja wake jijini Tanga mwishoni mwa wiki, na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali na viongozi wa serikali. **PICHA" MPIGAPICHA WETU**

# Kinana sasa ataka kero za W'biashara ofisini kwake

**Na Sabato Kasika**

MAKAMU Mwenyekiti wa CCM Bara, Abdulrahman Kinana, amewataka wafanyabiashara kuorodhesha changamoto zinazowakabili na kumfikishia ofisini kwake Mei 5 mwaka huu ili azifanyie kazi.

Kinana alitoa agizo hilo jijini Dar es Salaam juzi, katika maadhimisho ya miaka 18 ya mafanikio ya kampuni ya kusafirisha mizigo baharini ya Silent Ocean Ltd, iliyohudhuriwa na wafanyabiashara na watu wa kada mbalimbali.

"Pamoja na kuleta changamoto hizo kwangu, zifikisheni pia kwa waziri husika, lakini mimi nitafuatilia kwa karibu ili kuhakikisha changamoto zinazowakabili zinatatuliwa," alisema Kinana.

Alikiri kwamba wafanyabiashara wanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwamo sheria ambazo si rafiki kwao, hali ambayo inachangia kuwafanya washindwe kufanya biashara zao kwa ufanisi.

"Nchi hii imeharibiwa na vikao, nchi imeharibiwa na mchakato, nchi imeharibiwa na tuko mbioni, nchi imeharibiwa na tutaifanyia kazi na nchi imeharibiwa na tupeni muda na nchi hii imeharibiwa na tutawasikiliza, yote tumeshayasikiliza tunataka vitendo," alisema.

Aidha, Kinana aliipongeza Silent Ocean Ltd na Kilimanjaro Star Cargo kwa kufungua ofisi Marekani ili kwamba mtu anayetaka kusafirisha mizigo kutoka huko hadi nchini aweze kupata huduma hiyo.

Awali, Mwenyekiti wa wafanyabiashara Mkoa wa Dar es Salaam, Yusuph Yenga, aliishikuru serikali kwa kukusanya kodi bila kutumia nguvu, na kwamba wafanyabiashara wanafurahia hatua hiyo.

"Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), imetufurahisha kwa hatua hiyo, lakini changamoto bado iko bandarini ambapo utoaji wa mizigo unachukua muda mrefu kuanzia wiki mojan hadi tatu," alisema Yenga.

Aliiomba serikali iwasaidie kumaliza tatizo hilo, huku Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT), akitaka wamachinga kuondolewa mbele ya maduka ya wafanyabiashara wakubwa Kariakoo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, iliwataka wafanyabiashara kuipa serikali ushirikiano wakati ikiendelea kuwaboreshea mazingira ya biashara.

"Serikali inatambua changamoto zenu inafanya jitihada za kuweka mazingira rafiki ya kufanya biashara, lakini pia kuwe na jukwaa la kukaa na kuzijadili," alisema Bashungwa na kuongeza:

"Lakini pia mmegusia suala la wamachinga kwamba wanaziba maduka yenu Kariakoo, ninyi wote ni watoto wa serikali na ipo kwa ajili yenu itawajengea uwezo ili kufikia mafanikio."

Mkurugenzi Mtendaji wa Silent Ocean Ltd na Kilimanjoro Star Cargo, Mohamed Soloka, alisema wamefungua ofisi Marekani ikiwa ni mwendelezo wa kupanua huduma zao.

Ofisi yetu nchini Marekani ipo Washington DC, hivyo kwa wale wanaotala kusafirisha bidhaa zao kutoka kwenda nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania, tunaweza kuwahudumia," alisema Soloka.

# Spika awataka Wabunge kuichangamkia mikopo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amewataka wabunge kuchangamkia fursa ya huduma ya mikopo maalum ya muda mfupi iliyotangazwa na Benki ya NMB.

Dk. Tulia pia ameipongeza benki hiyo kwa hafla ya Iftari ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani iliyowaandalia Wabunge Ijumaa jijini Dodoma na kuhudhuriwa na viongozi wa dini, Serikali na waalikwa wengine, ambapo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, aliwakilishwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyohudhuriwa na watu zaidi ya 500, Spika Dk. Tulia aliishukuru NMB kwa kuwakutanisha kwa upendo, imani na mashirikiano makubwa na kwamba hafla hiyo imewapa Wabunge na waalikwa wengine nafasi ya kuendelea kujifunza kupitia Waislamu, namna ya kuishi nao.

"Jambo hili ni la heri sana, na tunaamini Mwenyezi Mungu atawabariki sana NMB kwa hiki mlichofanya. Ingawa lengo la Iftari hii ilikuwa ni kufuturisha wabunge, lakini kuna waalikwa wengine wengi wako hapa, tunawashukuru nao kwa kuungana nasi, lakini zaidi kwenu nyie NMB mliofanikisha jambo hili.

"Hapo mmesema jambo la ziada kuhusu uwapo wa huduma ya mikopo maalum ya muda mfupi, ambayo mnatukaribisha wabunge tuje kukopa, kwa kipindi cha miezi mitatu ya vikao vyetu, ili wabunge tuishi kwa malengo.

"Naamini wabunge wengi watakuja kutumia fursa ya kukopa ili kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao na kutimiza malengo waliyojiwekea," alibainisha Spika Dk. Tulia.

Awali akimkaribisha Spika wa Bunge Dk. Tulia, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi alisema:

"Ramadhani ni kipindi ambacho familia, marafiki na jamii huja pamoja kuimarisha ukaribu na umoja wao, hii ni nguzo muhimu ambayo inatuimarisha kiimani na kutufanya wamoja.

"Kwa kuandaa futari hii, sisi kama NMB tunaendelea kudumisha ukaribu na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, viongozi wa Serikali ya Mkoa wa Dodoma na wateja wetu. Huu ni wakati mzuri kwa Waislamu na jamii kwa ujumla kutafakari juu ya upendo kwa familia zetu, shukrani kwa Mungu na toba za dhati.

Mponzi alibainisha kuwa hiyo ndio sababu ya NMB kulipa umuhimu mkubwa jambo hilo na kwa mwaka huu, tayari wameshatoa futari kwa mkoa wa Dar es Salaam, Dodoma na baadaye watafanya hivyo kwa Waislamu

# Asakwa tuhuma za mauaji kisha kufukia mwili kwenye shimo

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi mkoani hapa, linamtafuta mkulima wa Kijiji cha Barikiwa, Wilaya ya Liwale, Saidi Ngamila (30) kwa tuhuma za mauaji ya Mwajuma Lipala (49) kwa kumkata na kitu chenye ncha kali kisha mwili wake kuuzika karibu na eneo la nyumba yake na kutokomea kusikojulikana.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, ACP Mtatiro Kitinkwi, alisema hayo alipokuwa anazungumza na mwandishi wa habari hizi ofisini kwake na kueleza Mwajuma anadaiwa kuuawa mwishoni mwa wiki iliyopita.

Alisema, siku ya tukio Mwajuma akiwa na mume wake wa ndoa, Rahidi Mkumba (69), walienda shambani kwa ajili ya ujenzi wa banda litakalotumika kulinda mazao yao.

Kitinkwi alisema, wakati mume akiendelea kushughulika la ujenzi, mke alimuaga mumewe anakwenda kukata nyasi za kuezekea banda lao na hakurejea hadi alipogunduliwa akiwa ameshafariki dunia huku mwili wake ukiwa umefukiwa ndani ya shimo.

Alisema mume alipoona mke wake anachelewa kurudi ndipo aliamua kumfuatilia alikokuwa ameelekea bila mafanikio na kuamua kutoa taarifa kwa uongozi wa Serikali ya Kijiji.

Alisema walianza kumtafuta na kufanikiwa kuona viatu alivyokuwa amevaa na mundu aliyochukuwa kukatia nyasi.

Pia, alisema wakati wanakijiji wakiendelea kumtafuta Mwajuma, pembezoni mwa nyumba ya mtuhumiwa kulikutwa shimo ambalo linaonekana kuchimbwa siku za karibuni ndipo walipoamua kutoa taarifa Kituo cha Polisi Liwale mjini na walipofukua walikuta mwili ukiwa umefukiwa.


Kitinkwi alisema mwili huo ulikutwa ukiwa umetenganishwa kichwa na kiwiliwili na majeraha mengine kwenye mwilini.

Hata hivyo, alisema mtuhumiwa alitokomea kusikojulikana.

"Mtuhumiwa baada ya kufanya unyama huo ametoroka na tunaendelea kumsaka ili afikishwe kwenye vyombo vya utoaji haki kujibu tuhuma zinazomkabili," alisema Kitinkwi.

Pia, Kamanda alisema uchunguzi wa awali unaonesha mtuhumiwa Ngamila alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na marehemu Mwajuma, kauli ambayo imeungwa mkono na baadhi ya wakazi wa Kijiji cha Barikiwa.

HABARI KITAIFA




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wa pili (kulia),akimkabidhi mfano wa hundi mshindi wa kwanza katika mashindano ya Kimataifa ya kuhifadhisha Qur-aan, Abdulhakim Mohammed Ali, kutoka Yemen, mashindano hayo yameandaliwa na Jumuiya ya kuhifadhisha Qur-aan Tanzania chini ya Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Shekhe Othuman Kapolo (kushoto), na kudhaminiwa na Benki ya CRDB kitengo cha Albarakah chini ya Mkuu wa Kitengo hicho, Rashid Rashid (kulia), yaliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Prof. Ngowi: Zifahamu fursa zilizopo katika ujasiriamali

**Na Jenifer Gilla**

KATIKA mwendelezo wa mafunzo ya aliyekuwa Profesa wa Uchumi katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, marehemu Prof. Honest Ngowi, leo tunaangazia moja ya masomo ya kuziangalia fursa na kuzitendea haki.

Kwa mujibu wa Prof. Ngowi, Tanzania ni moja ya nchi zenye fursa nyingi zinazotokana na uwepo wa rasilimali za kutosha lakini bado wajasiriamali wengi wanashindwa kubaini fursa hizo na kuzitumia pamoja wa wito wa kuzichangamkia fursa hizo kutolewa kila kukicha.

Mchumi huyo kupitia chaneli yake ya Youtube ya Ngowi TV alizibainisha baadhi ya fursa zilizopo ili Watanzania wazifahamu na kuzitumia na kuzitendea haki.

Alisema fursa zimekuwa zikizunguka jamii katika nyanja mbalimbali, akitolea mfano wa kugunduliwa kwa gesi ya Mtwara, Serikali kuhamia Dodoma, sera za viwanda, bajeti za serikali, isipokuwa uwezo wa jamii kuzigundua fursa hizo bado ni mdogo.

Alisema utafiti wa uchumi nchini unaonyesaha kuwa suala la fursa kwa wajasiriamali ni mtambuka na lilianza kutambulika miaka ya 1967 na kushika kasi miaka ya 1980 kutokana na kuwa huko nyuma halikuwapo kutokana na sera ya ujamaa iliyokuwapo haikuupa kipaumbele.

Alifafanua kuwa kuna fursa za muda mrefu na za muda mfupi, za moja kwa moja na ambazo sio za moja kwa moja,fursa kubwa na ndogo, hivyo muhimu mjasiriamali kuzifahamu.

"Hivyo kabla mjasiriamali hajaamua kuzichangamkia fursa ni muhimu afanye uchambuzi ili ajue kuwa fursa inayotangazwa ni ya muda mfupi au mrefu, kubwa, ndogo au ya kati, haya yote yatamsaidia kuitendea haki fursa hiyo," alisema Prof Ngowi.

Alisema kuwa sio kila mmoja anayeweza kuziona fursa lakini sifa kuu ya mjasiriamali ni uwezo wa kuziona, pale ambapo mtu anakimbia kitu, mjasiriamali huona kitu.

"Pale ambapo mtu hukimbia kitu au mahali kwa sababu ya ukame, mjasiriamali anaona fursa ya kwenda kufanya biashara ya kuuza maji, wakati mwingine anaona kuwa hawezi kuishi pale kwa sababu hakuna huduma ya hoteli mjasiriamali anaona fursa ya kwenda kufungua biashara ya hoteli, chakula na maji," alifanua.

Vilevile mchumi huyo alisema kuwa fursa hupatikana kulingana na mahitaji ya watu. Mjasiriamali anapaswa kuangalia elimu, utamaduni na uhalisia wa jamii fulani ndipo kujua ni fursa gani inapatikana.

Prof Ngowi alisema kuwa hata katika pale bajeti ya nchi inaposomwa kunapatikana fursa za biashara za aina mbalimbali ikiwamo ujenzi wa barabara, ujenzi wa shule, biashara katika miji.

"Mfano bajeti zinapokuwa zinasomwa kuhusu maendeleo ya barabara wewe kama mkandarasi unaona fursa gani ya kupata fungu katika hiyo.Huwa nawauliza wanafunzi wangu bajeti ya nchi inaposomwa bil 29.5 je, wewe unaona fursa gani," alisema.

Alisema pia hata katika bajeti za halmashauri zilizotengwa kuna fursa za biashara ambazo kwa kiasi kikubwa zinatekelezwa na sekta binafsi na wajasiriamali, kwa hiyo ni muhimu kutembelea humo.

Aliongeza kuwa fursa nyingine kwa sasa zinapatikana katika sekta ya usafirishaji kwa kuwa sasa hivi usafiri wa abiria umekuwa na changamoto, na pia kwenye migahawa kwa kuwa ni hitaji la muhimu.

Kwa mujibu wa Prof Ngowi msimu wa vijana kuhitimu elimu ya juu pia unakuwa na fursa za ujasiriamali kama vile kuuza mataji ya kuvalisha watunukiwa, kupiga picha, na kufanya matangazo ya biashara.

Alisema kuwa kuwapo na fursa hakutobadilisha maisha ya mjasiriamali kama hatozitendea haki, kwa hiyo ni muhimu mjasiriamali anapoziona fursa hizo kuzichangamkia na kuzitumia ipasavyo.

"Tusipozichangamkia na kuzifanyia kazi fursa hizo tunasema kwamba ni loss of opportunity (kupoteza fursa), kwa hiyo kuna mambo ya msingi ambayo wajasiriamali wanapaswa kuyafanya katika fursa hizo," alisema.

Aliongeza kuwa mjasiriamali anatakiwa kuwa tayari kwa fursa wakati wowote ili zisimpite na ili hilo litokee anapaswa kukaa kimkakati ikiwamo kuwa na mipango, maono na malengo.

# Wawili wafariki dunia kwa kugongwa na basi

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU wawili wakazi wa mji mdogo wa Masoko, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi, wamekufa papo hapo baada ya pikipiki waliyokuwa wakisafiria kugongwa na basi.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, ACP Mtatiro Kitinkwi, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kwamba imetokea Kijiji cha Nangurukuru Kilwa, Aprili 20, mwaka huu, saa 11:15 asubuhi, barabara kuu ya Kibiti-Lindi.

Aliwataja marehemu hao kuwa ni dereva wa pikipiki, Jafari Madega Kizenga (30) na mtumishi wa Shirika la Umeme (TANESCO), Wilaya ya Kilwa, Athumani Madega (58), wote wakazi wa mji mdogo wa Masoko.

Kitinkwi alisema watu hao walikuwa wakisafiri na pikipiki yenye namba za usajili MC 109 CPX iliyokuwa ikiendeshwa na Jafari Kizenga na kugongwa na basi lenye namba za usajili T.501 BRU lililokuwa likiendeshwa na Saidi Mohamedi Saidi (40), mkazi wa Manispaa ya Lindi.

Alitaja chanzo cha ajali ni mwendesha pikipiki kukatisha barabara kutoka upande mmoja kwenda mwingine wakati basi likiwa linafanya safari kutokea mkoani Mtwara kwenda jijini Dar es Salaam.

Kamanda alisema dereva wa basi anashikilia kwa mahojiano na atafikishwa mahakamani kujibu shtaka linalomkabili baada ya uchunguzi kukamilika.

"Uchunguzi wetu wa awali unaonyesha huyu mwendesha pikipiki alikuwa amekuja kutoka upande wake kwenda ule wa basi," alisema Kitinkwi.

# Ripoti: Mazingira rafiki yawepo shuleni kufikia ubora wa elimu

**Na Christina Mwakangale**

IMEBAINISHWA, ili kukuza ubora wa elimu nchini, wasimamizi wa elimu wahakikishe wanafanya ukaguzi wa shule mara kwa mara, kuweka mazingira rafiki ya ujifunzaji ikiwamo milo kupatikana katika shule za msingi, hususan vijijini.

Kadhalika, jamii imepewa wito wa kujiunga na kuhamasika katika kusaidia serikali kutatua baadhi ya changamoto katika sekta ya elimu, kama vile upungufu wa madawati na uhaba wa matundu ya vyoo na mabweni. Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) 2021, imebainisha hayo kwenye kipengele cha haki ya kupata elimu, iliyozinduliwa hivi karibuni jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga.

"Utafiti mbalimbali umeonyesha kuwa umbali mrefu kwenda shule una athari hasi katika ufaulu wa elimu ya mwanafunzi. Kutumia muda mrefu kwenda shule pia kunachangia mahudhurio yasiyo ya kawaida shuleni na kujenga mazingira ya kuacha shule.

"Kwa sababu ya umbali mrefu kwa kawaida watoto hufika shuleni wakiwa wamechoka, jambo ambalo huwaathiri kujifunza na kupunguza muda wao wa kujifunza pamoja na kuwa na umakini. Umbali wa shule ni sababu ya mahudhurio duni shuleni na kuacha shule," inabainisha ripoti hiyo.

Ripoti inabainisha kwamba, utafiti uliofanyika katika Wilaya ya Rorya mkoani Mara, ulionyesha umbali mrefu unasababisha kupungua umakini kwa wanafunzi, walimu na wakati mwingine ukosefu wa mlo shuleni husababisha wapate vidonda vya tumbo, maumivu ya kichwa kwa kuwa wengi wao hawawezi kurudi nyumbani kupata mlo wa mchana.

"Tatizo la uchovu na kutozingatia ujifunzaji darasani linaweza kuchangiwa na ukosefu wa chakula shuleni na ukweli ni kwamba watoto wa shule hawawezi kurudi nyumbani kupata chakula na kurejea shuleni. "Desemba 2021, wanafunzi 50 kutoka Kata ya Boko Mnemela mjini Kibaha, Mkoa wa Pwani, inadaiwa hawakuweza kuhudhuria shule kutokana na kutakiwa kulazimika kutembea umbali wa hadi kilomita tisa kufuata masomo,"

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stars ikijipanga mapema inaweza kufuzu AFCON 2023

**TAYARI** Shirikisho la Soka Afrika (CAF), limepanga makundi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, zitakazofanyika nchini Ivory Coast.

Kwa upande wa timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars imepangwa Kundi F na Uganda, Niger pamoja na vigogo vya soka Afrika, Algeria ambao walitwaa ubingwa huo mwaka 2019 nchini Misri baada ya kuifunga Senegal katika mechi ya fainali.

Katika kila kundi kati ya 12, timu mbili zitakazoshika nafasi ya juu zitakata tiketi ya kwenda kushiriki fainali hizo za juu kabisa kwa ngazi za kimataifa barani Afrika ambazo mwakani zitafanyika kwa mara ya pili nchini Ivory Coast tangu kuanzishwa kwake 1957.

Katika Kundi hilo la F, tayari wengi wanaona nafasi iliyobaki kwa Stars ni moja ambayo itaipigania na Uganda pamoja na Niger huku nyingine wakiitoa moja kwa moja Algeria ambayo imetwaa taji hilo mara mbili, mwaka 1990 na 2019.

Hiyo ni kutokana na ukubwa, uzoefu, uwezo na ubora wa kikosi cha Algeria kinachoundwa na wacheji wengi wanaocheza soka la ushindani barani Ulaya, lakini pia na mlolongo wao wa kufanya vizuri katika michuano hiyo ambayo wametwaa ubingwa mara mbili.

Hata hivyo, pamoja na ukweli huo, bado sisi tunaamini katika soka lolote linaweza kutokea kutokea ndani ya dakika 90 kama maandalizi mazuri yataanza kufanyika sasa kwa kila mmoja kutimiza majukumu yake ndani na nje ya kikosi cha Stars.

Imani hiyo tunaipata hasa tukivuta kumbukumbu za hivi karibuni kwa Stars kufanya vizuri ugenini kwa kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya DR Congo, ambao ni miongoni mwa timu imara na zinazoundwa na nyota wengi wanaocheza soka la kulipwa Ulaya.

Stars ilimudu kutoka sare hiyo katika mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar baadaye mwaka huu, tena ikiwa haina nyota wake tegemeo, Mbwana Samatta, jambo ambalo linatufanya kuamini katika maandalizi ya mapema na wachezaji kutia nia ya kupambana mwanzo mwisho.

Kwa maana hiyo, hata mechi dhidi ya Algeria, kama Stars ikiandaliwa mapema na wachezaji wakijengewa kujiamini, hakuna kitakachoshindikana ndani ya dakika 180 kwenye mechi ya nyumbani na ugenini.

Kinachotakiwa ni Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Kim Poulsen, kuanza kupanga mikakati yake na kuiwasilisha mapema kwa waajiri wake Shirikisho la Soka nchini (TFF), ili kufanyiwa kazi, lakini pia mashabiki na Watanzania kwa ujumla kuwa bega kwa bega katika kuziunga mkono juhudi hizo.

Tunaamini Stars ina uwezo mkubwa wa kupata matokeo ikiwa katika uwanja wake wa nyumbani wa Benjamin Mkapa, kama Watanzania kwa ujumla watakuwa mstari wa mbele katika kuwahamasisha wachezaji kwa kaulimbiu ambayo imekuwa ikiimbwa na mashabiki wa Simba ya 'Kwa Mkapa Hatoki Mtu'.

Ni wazi kama itaweza kukusanya alama tisa na nyumbani na kwenda kutafuta angalau mbili tu ugenini, inaweza kuwa moja kati ya timu mbili zitakazofuzu fainali hizo kutoka Kundi F, hivyo wakati wa maandalizi ni sasa.

Kinachotakiwa kwa sasa pia ni Poulsen kuzidi kumulika wachezaji hususan wanaocheza soka la kulipwa nje ya Tanzania kwa kuwapa nafasi zaidi kila anapoita kikosi kwa ajili ya mechi za kirafiki kama alivyofanya kwenye Kalenda ya Fifa iliyopita.

Lakini pia TFF haina budi kuhakikisha katika kila Kalenda ya Fifa, Taifa Stars inacheza mechi za kirafiki mbili ama tatu na moja kati ya hizo ikicheza ugenini ili kuwajengea wachezaji kujiamini wanapocheza nje ya uwanja wao wa nyumbani.

Lengo letu ni kuona Tanzania ikifuzu kwa mara ya tatu katika historia yake kushiriki michuano hiyo, lakini pia ikiigeuza kuwa kawaida kwake kushiriki kila msimu kabla ya kuanza kuweka malengo makubwa ya kufika nusu fainali na hatimaye kubeba ubingwa huo.

Hili litawezekana tu kama maandalizi yatakuwa yakifanyika mara tu kila fainali za msimu husika zitakapomalizika kwa kila mmoja kubeba vema majukumu yake kuanzia viongozi, kocha na wachezaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kuisaka AFCON 2023 wachezaji wasichaguliwe kimazoea

Na Adam Fungamwango

**TAYARI** Watanzania wote wanajua kuwa timu yao ya Taifa, Taifa Stars imepangwa Kundi F kuelekea kufuzu fainali za Kombe la Mataifa Afrika (AFCON), zitakazofanyika mwakani nchini Ivory Coast.

Baada ya droo iliyochezeshwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), lenye Makao Makuu yake nchini Misri, Stars iliwekwa kwenye kundi moja na timu za Algeria, Uganda na Niger.

Ni kweli kuwa si kundi jepesi kwa sababu Algeria ni moja kati ya timu vigogo vya soka barani Afrika, huku Uganda ikiwa timu ambayo kwa kawaida inaipa shida sana Tanzania upande wa soka kwenye mechi zote za timu za wakubwa, vijana chini ya miaka 23, 20, 17 na hata timu za wanawake.

Takwimu zinaongea kuwa Uganda ilikuwa mlima rahisi kwenye mechi ambayo Stars ilishinda na kwenda fainali za AFCON 2019 nchini Misri, lakini kabla ya hapo ulikuwa ni mlima mkubwa mno.

Kihistoria tu ni mara chache sana kwa Tanzania kuifunga Uganda kuliko wao kuifunga Stars. Kama ingekuwa ni Kenya, angalau.

Niger ni timu ambayo kwenye makaratasi inaonekana kama ni timu mchekea, lakini sivyo. Kwa sasa soka la Afrika Magharibi limekuwa na kuenea sana. Ni kama wameambukizana. Zamani Afrika Magharibi timu tishio zilikuwa ni Nigeria, Ghana na Cameroon, lakini baadaye zilianza kuja timu kama Ivory Coast na kufuatia na zingine mpaka zile nchi ndogo ndogo nazo kwa sasa zimekuwa na wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa Ulaya, huku nchi za ukanda huo zikiwa zimeendelea kwa kuweka akademi nyingi za michezo.

Ni kwamba wachezaji wa mwanzo wa kulipwa kwenye nchi za Afrika Magharibi wengi wametengeneza akademi zao kwa kuzisambaza kwenye nchi mbalimbali jirani, hivyo nchi kama Niger si ya kubeza kwani ina wachezaji wenye vipaji vikubwa.

Hata hivyo, hakuna cha kuhofia kwa Stars kama itaanza maandalizi mapema na ya uhakika. Pamoja nayo, ni kwamba ili Watanzania tufuzu ni lazima uchaguzi wa wachezaji ufanywe kwa makini.

Simfundishi Kocha Mkuu, Kim Paulsen kazi, kwa sababu ndiyo kazi yake, lakini ni kwamba wachezaji wasichaguliwe kimazoea.

Tumeaona huko nyuma baadhi ya wachezaji ambao wamefanya vema na sasa hata kwenye timu zao hawapangwi, lakini wamekuwa wakiitwa.

Ili tufuze kwa sasa, umakini unatakiwa kwa kuita wachezaji ambao wanafanya vema kwa sasa na si kwenye klabu kubwa, hata zile ndogo. Hatupaswi kung'ang'ania wachezaji kutokana na majina yao kwa yale waliyoyafanya zamani.

Mfano mchezaji George Mpole, anaichezea Geita Gold, amechaguliwa kwa mara ya kwanza tu, lakini vitu alivyovifanya ni hatari na mfano wa kuigwa. Wala huwezi kuamini bado ni mchanga kwenye kikosi hicho.

Aziz Andambwile wa Mbeya City, ilifika wakati kwenye mechi za Stars zilizo kwenye Kalenda ya FIFA zilizocheza hivi karibuni alikuwa akishangiliwa na mashabiki uwanja mzima, kila anapogusa mpira.

Tumeona pia kuna baadhi ya wachezaji wapya kutoka nje ya nchi, ambao nao kama taratibu zitafanyika wanaweza pia kuongeza nguvu kwenye kikosi hicho.

Paulsen ameonekana kubadilika kwa sasa kwenye kuchagua wachezaji katika mechi hizi, lakini isiwe kwenye mechi za kirafiki na kwenye mashindano halisi akachukua wachezaji kwa majina yao au klabu zao.

Kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa sasa ukitazama, ukiondoa washambuliaji, kuna timu zina wachezaji wazuri sana, ambao wanachokosa ni mafunzo kidogo tu ili viwango vyao viwe wazi zaidi.

Nina uhakika, kwa kikosi nilichokiona kwenye mechi dhidi ya Afrika ya Kati na Sudan na kiwango kile, kama wataongezwa baadhi ya wachezaji wanaofanya vizuri kwenye Ligi Kuu, fainali za AFCON 2023, Stars inaweza kuwamo.

HABARI KITAIFA

# CCM yawaonya viongozi wanaosumbua bodaboda

**Na Mwandishi Wetu,** IRINGA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewaonya viongozi wanaosababisha usumbufu kwa madereva wa bajaji na pikipiki za kubeba abiria, maarufu bodaboda, kikisisitiza kuwa hakitawafumbia macho.

Angalizo hilo lilitolewa jana mjini hapa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa chama hicho (UVCCM), Kenani Kihongosi, alipohutubia maelfu ya vijana wakati wa kongamano la vijana kuhusu faida za kugombea nafasi mbalimbali ndani ya chama na jumuiya zake, umuhimu wa sensa pamoja na uzinduzi wa nyumba ya Katibu wa UVCCM Mkoa wa Iringa.

Kihongosi alisema kundi hilo lisihesabike kama wahalifu kwa kuwa linatambulika rasmi kitaifa, akitolea mfano uamuzi wa serikali ulioanza kutekelezwa Julai Mosi mwaka jana wa kupunguza faini za makosa ya barabarani dhidi ya madereva wa bajaji na pikipiki.

"Vijana wenzetu wa bajaji na bodaboda siyo wahalifu, ni vijana wanaojitafutia riziki na ndiyo maana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan aliwasaidia na kupunguza faini zao kutoka Sh. 30,000 hadi Sh. 10,000.

"Hivyo, niwaombe wale wote wenye dhamana kuhakikisha wanawasaidia vijana hawa na siyo kutoa matamko ambayo yanavunja moyo vijana wenzetu.

"Tunaomba pia wajue kuwa hawa bodaboda na bajaji hawana tofauti na vijana wengine ambao wamejiajiri katika ofisi au shughuli mbalimbali na hawa vijana vyombo vyao vya moto ndiyo ofisi zao.

"UVCCM tutasimama imara kuwalinda vijana wenzetu kwani wajibu wetu ni kuwa sauti ya vijana wa Taifa hili," Kihongosi alionya.

Katibu Mkuu huyo pia alisema wanamuunga mkono Rais Samia, hivyo hawatamfumbia macho kiongozi yeyote atakayeonekana kutaka kumchonganisha Mkuu wa Nchi na vijana. "Vijana tutakuwa wakali kwa wale watakaoleta chokochoko dhidi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na serikali yake," Katibu Mkuu wa UVCCM alionya.

Kihongosi pia alitoa rai kwa vijana kujitokeza kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi iliyopangwa kufanyika Agosti mwaka huu, akisisitiza kuwa sensa hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Alisema UVCCM wanampongeza kwa dhati Chifu Hangaya ambaye ni Rais Samia kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ya kuwatumikia Watanzania.

"Katika kuhakikisha sekta ya utalii inakua na kuongeza Pato la Taifa tumeshuhudia amezindua filamu inayoitwa Royal Tour itakayoliingizia taifa fedha za kigeni kutokana na watalii ambao watakuja kutembelea vivutio nchini, hatua hii ni kubwa toka nchi ilipopata uhuru," alisifu.

**RUSHWA CCM**

Kiongozi huyo wa CCM pia alikemea vitendo vya rushwa, akionya kuwa chama hakitamfumbia macho kiongozi au mwanachama yeyote atakayebainika kuendekeza vitendo hivyo wakati wa uchaguzi wa ndani ya chama.

"Kila mwanachama, akiwamo kijana, anao wajibu wa kutumia haki yake ya msingi kugombea. Mwenyekiti CCM Taifa (Rais Samia) na chama kinatutaka vijana kuamka na kugombea," alisema.

Awali, akiwasilisha taarifa ya Kamati ya Siasa ya Mkoa, Katibu wa CCM Mkoa wa Iringa, Rukia Mkindu, alisema katika kipindi cha Januari hadi Aprili 2022, mkoa una jumla ya wanachama wapya waliojiunga na CCM 2,704.

Aliishukuru serikali kwa kuupatia Mkoa wa Iringa Sh. bilioni 8.86 zilizotokana na mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19, fedha hizo zikitumika katika ujenzi wa miundombinu ya afya na elimu.

Alibainisha kuwa madarasa 245 yamejengwa katika shule za sekondari, madarasa 82 shule za msingi (shikizi) na mabweni mawili kwa watoto wenye uhitaji, pia ujenzi wa vituo vya afya katika wilaya mbalimbali za mkoa huo.

**VIJANA KUTUMIKA**

Hassan Makoba, Katibu wa UVCCM Mkoa wa Iringa, alitaja kero zinazowakabili ni pamoja na baadhi ya viongozi wa matawi ambao siyo waaminifu kuficha fomu za kuwania nafasi mbalimbali na baadhi ya viongozi kuwatumia vijana kupanga safu kwa maslahi yao binafsi.




Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid akiwakabidhi sehemu ya sadaka ya Mwezi Mtukufu wa Ramadhani wawakilishi wa watoto wanaolelewa katika Kituo cha Watoto Yatima cha Mazizini, Unguja Zanzibar ikiwa ni sadaka iliyotolewa na Benki ya CRDB kwa baadhi ya vituo. Katikati ni Ofisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya CRDB, Fredrick Nshekanabo.. **PICHA: JMPIGAPICHA WETU**

# Sensa yakamilika kwa asilimia 80

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi mwaka huu yamefikia asilimia 80, huku ikisisitiza kuwa itahakikisha ifikapo Agosti 23 yatakuwa yamekamilika kwa asilimia 100.

Aidha, imesema sensa ya mwaka huu itafanyika kidijitali hivyo itakuwa mfano kwa nchi nyingi za Afrika kuja kujifunza namna ya kuendesha zoezi hilo.

Akizungumza jana jijini hapa Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Anne Makinda, wakati akifungua mafunzo ya waratibu wa sensa ngazi ya Mkoa na Wilaya alisema serikali imedhamiria kufanya sensa kidijitali.

"Sensa ya mwaka huu inaenda kufanyika kidijitali zaidi ndio maana tumeandaa mafunzo haya ya siku mbili kwenu ninyi waratibu kwa sababu tunaamini mnahusika moja kwa moja katika kuhakikisha zoezi hili linafanyika kwa ufanisi zaidi,"alisema

Makinda aliwataka waratibu hao kuhakikisha wanatanguliza uzalendo katika kufanikisha zoezi hilo hasa kipindi cha kuchagua makarani na wasimamizi wa zoezi hilo mbalo mara nyingi dosari hutokea.

"Ni marufuku kuweka undugu katika zoezi la kutafuta makarani na wasimamizi wa sensa, ni vyema mkatanguliza uzalendo pia kuna vifaa vya sensa mtakavyopewa mkavitunze na baada ya zoezi kumalizika virejeshwe mahali husika haitaleta picha nzuri kuona mtu anapewa vifaa anatumia hivyo hivyo mwisho wa siku vinapotea au kuharibika,"alisisitiza

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, alisema maandalizi ya sensa ya watu na makazi yamefikia asilimia 80 bado asilimia 20 ambazo hadi kufikia Agosti 23 mwaka huu siku ya sensa yatakuwa yamekamilika kwa asilimia 100.

## Wataka mpango kusaidia wanaougua haemophilia

**Na Beatrice Shayo**

SERIKALI imeshauriwa kuweka mpango mkakati kwa ajili ya kusaidia wenye ugonjwa wa haemophilia nchini, badala ya kutegemea msaada wa dawa na vifaa kutoka nje ya nchi.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Daktari Bingwa wa magonjwa ya damu katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) na Rais wa Chama cha Haemophilia Tanzania (HST), Dk. Stella Rwezaura, wakati wa mkutano mkuu wa chama hicho.

Alisema wameishirikisha Wizara ya Afya kuliangalia jambo hilo kwa sababu dawa hizo huuzwa kwa gharama kubwa.

"Kuna kichupa kimoja kinauzwa Sh. milioni 10 na mgonjwa anahitaji kama vitatu kwa mara moja." alisema

Alisema mpaka sasa wagonjwa wenye Haemophilia wapo 172 ambao huwatibia kwa msaada wa Shirika la Haemophilia la Dunia na mgonjwa mmoja kwa makadario ya chini ni Dola za Kimarekani 100,000 kwa mwaka mmoja. Alisema serikali haijaanza kununua dawa za ugonjwa huo wanapata msaada kutoka Shirika la Haemophilia la Dunia na wanapoomba dawa huwasilisha idadi ya wagonjwa.

Alisema idadi ya wagonjwa hao ni wachache waliotambulika na mkakati wao ni kwenda kuwaibua ili wapatiwe matibabu. "Kati ya watu 10,000 mmoja anaweza akawa na Haemophilia tunategemea kuwa na wagonjwa 6,000 ama zaidi tunaendelea kuwatafuta, ili waweze kupatiwa matibabu maana wanaokuja Muhimbili kupatiwa matibabu ni 172,"alisema.

Dk. Rwezaura alisema kuna wengine wapo mikoani hawajaweza kuwafikia na hata wanapofikishwa katika vituo vya afya kuna wataalamu bado hawajaujua huu ugonjwa.



Wanafunzi wa klabu za Maji na Usafi wa Mazingira kutoka Shule za Sekondari Zanaki na Kibasila jijini Dar es Salaam wakiwa katika mtambo wa uzalishaji maji Ruvu Chini katika ziara yao ya mafunzo. Klabu hizo zinaratibiwa na Mamlaka ya Maji Safi na Utunzaji wa Mazingira (DAWASA). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Askofu Getrude Rwakatare apata mrithi

**Na Joseph Mwendapole**

ROSE Mgetta ambaye amesimikwa rasmi kuwa Askofu Mkuu wa Makanisa ya Mlima wa Moto Mikocheni 'B' mkoani Dar es Salaam kuchukua nafasi ya Mwasisi wa Kanisa hilo, Askofu Getrude Rwakatare amepongeza kazi kubwa zinazofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Dk. Rwakatare ambaye alianzisha Kanisa hilo mwaka 1993 alifariki dunia mwaka 2020 na tangu wakati huo Askofu Rose amekuwa akikaimu nafasi yake hadi Jumamosi aliposimikwa rasmi.

Ibada ya kumsimika Rose iliendeshwa na Askofu wa Makanisa ya ELIM Pentecoste Tanzania, Peter Konki, kwenye Kanisa la Mlima wa Moto Mikocheni 'B' mkoani Dar es Salaam na kuhudhuriwa na waumini wa kanisa hilo na wageni mbalimbali.

Akizungumza mara baada ya kusimikwa rasmi, Askofu Rose aliushukuru uongozi wa Kanisa hilo kwa kuamini kwamba anaweza kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi na kuamua kumsimika rasmi kumrithi Dk. Rwakatare.

Alisema wanawake wanaweza kufanya mambo makubwa wakipewa nafasi tofauti na fikra za baadhi ya watu waliokuwa hawaamini kwamba mwanamke anaweza kuwa kiongozi kwenye nafasi kubwa na kufanikiwa.

"Mfano Rais Samia Suluhu Hassan wakati anaingia madarakani baadhi ya watu walikuwa na hofu kwamba huenda asimudu nafasi hiyo lakini sote ni mashuhuda wa namna alivyomudu majukumu yake na nchi inakwenda vizuri sana," alisema Askofu Rose.

Alisema amekaimu nafasi hiyo kwa miaka miwili tangu kifo cha mwasisi wa kanisa hilo, Dk. Getrude Rwakatare mwaka 2020 na baada ya kufanya kazi nzuri ya utumishi waumini na uongozi wa kanisa umeona kwamba anafaa.

Aliwaomba watanzania kushikamana na kuendelea kuishi kwa amani na upendo na kwamba viongozi wa dini kwa upande wao waendelee kutimiza wajibu wao wakuombea amani na kuwaombea viongozi wa nchi.

"Mwasisi wa Kanisa hili Dk. Rwakatare alinilea vizuri sana na nilikuwa chini yake kwa muda mrefu ni mtu alipenda kuwainuia wanawake na mmoja wa wanawake aliowainua ni mimi hivyo nawaahidi waumini wa kanisa kazi iliyotukuka," alisema Askofu Rose

Mtoto wa kwanza wa Dk. Rwakatare, Dk. Rose alisema Askofu huyo ana uzoefu wa kutosha kwani alifanyakazi kwa karibu sana na mwasisi wa kanisa hilo kwa muda mrefu akiwa msaidizi wake wa karibu.

"Sisi tumeona huyu ndiye anaimudu kazi hii kwa sababu ameifanya kwa muda mferu akiwa na mama yetu na waumini wameahidi kuendelea kumpa ushirikiano kwa sababu wanamwamini na wamekuwa naye siku zote," alisema Dk. Rose

Dk. Rose alisema waumini wa kanisa hilo wataendelea kuliombea taifa lizidi kuwa na amani wakati wote na aliwaomba watanzania waendelee kushikamana na kuishi kwa upendo ili kuhakikisha mshikamano uliopo unakuwa endelevu kwa ustawi wa taifa kwa ujumla.

# 'Ushiriki sekta binafsi muhimu kwenye kilimo'

**Na Mwandishi Wetu**

KITUO cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT) kimebainisha kuwa ushiriki wa sekta binafsi kwenye sekta ya kilimo unahitajika kwa kiasi kikubwa ili kuongeza uzalishaji na kufanya kilimo cha kisasa.

Akizungumza kwenye mkutano uliofanyika kwa njia ya mtandao wenye mada ya "Mapinduzi ya kilimo na umuhimu wa kugawa vitendea kazi kwa maofisa ugani kilimo" Mkurugenzi Mtendaji wa SAGCOT, Geoffrey Kirenga, mbali ya kuipongeza serikali kwa kugawa vitendea kazi hivyo, aliizungumzia namna sekta binafsi inavyoweza kutoa mchango mkubwa kwenye kuinua sekta ya kilimo nchini. "Kwanza naipongeza serikali kwa tukio kubwa la kugawa vitendea kazi kwa maofisa ugani wetu, lakini hii haiondoi ukweli kwamba sekta ya kilimo na sekta binafsi ni sekta ambazo zinashabihiana hasa kwenye kuongeza tija, kutafuta masoko na hata kwenye upatikanaji wa mitaji," alisema Kirenga.

Alisema ndani ya sekta binafsi kuna ujuzi, maarifa, mawasiliano na mitaji ambapo ili kuwa na kilimo chenye tija lazima uwe na vitu hivyo vya msingi ambavyo ni muhimu kuwafikia wakulima.

"Katika nchi zilizoendelea sekta binfsi inakuwa mstari wa mbele kwenye kupeleka ujuzi, maarifa, mawasiliano na mitaji jambo ambalo ni zuri hata kwa sisi kuliangalia kwa makini ili kilimo kiwe na tija endelevu," alisema.

"SAGCOT tutaendelea kuwa kiunganishi kati ya wawekezaji wa kilimo, makampuni na wakulima wenyewe kwenye kutafuta mitaji na masoko ya ndani na nje ya nchi kwa kushirikisha diaspora waliopo mataifa mbalimbali."

Alimtolea mfano Khadija Jabir kama moja ya watu ambao wamefanya nae kazi tangu akiwa mdogo akianza shughuli za kilimo cha mboga na matunda mpaka kufikia kuwa mkulima ambaye Rais Samia Suluhu Hassan alimtaja na kumtambua kama kijana wa mfano, na kuwataka vijana wengine kuiga na kujifunza ili kufikia malengo yao.

"Kuna kitu cha kujifunza kwa vijana wetu kupitia hawa wawekezaji wanapokuja nchini, kama alivyofanya Khadija, ambaye alianza akiwa mdogo mpaka kafikia kuwa mkulima mkubwa na wa mfano kwa vijana wengine nchini," alisema Kirenga.

# Sekta binafsi yajitosa dhidi ya vita ujangili

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TAASISI ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF)imeanza kuisaidia Serikali katika mapambano ya uwindaji haramu na usafirishaji wa wanyamapori kwa kuvidhibiti vitendo hivyo ikiwa ni njia mojawapo ya kukuza sekta ya utalii na kuongeza mchango wake katika pato la Taifa.

Kupitia mpango huo, TPSF imetoa mafunzo juu ya kudhibiti vitendo vya uwindaji haramu na usafirishaji wa wanyamapori pamoja na uhifadhi wa mazingira kwa wadau wake wote wa sekta binafsi Tanzania Bara na Visiwani.

Mkakati huo umetangazwa na Mchambuzi wa Sera kutoka TPSF, Victoria Michael, wakati akiwasilisha mada kuhusu nafasi ya sekta binafsi katika kusaidia uhifadhi wa maliasili kwenye mafunzo yaliyotolewa kwa njia ya mtandao kwa waandishi wa habari za uhifadhi.

Mafunzo hayo yametolewa na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) kupitia mradi wa Tuhifadhi Maliasili unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Watu wa Marekani (USAID).

Alisema uamuzi wa TPSF kuisaidia Serikali katika kudhibiti biashara hiyo haramu unatokana na washirika wakubwa wanaotoka katika sekta hizo binafsi kwa kushirikiana na baadhi ya wananchi katika kushiriki vitendo vya ujangili wa wanyamapori.

" Vitendo vya ujangili au uhalifu wa wanyamapori sio jambo jepesi kama tunavyolifikiria, bali ni kitu kinachohusisha zaidi ya sekta moja, ikiwemo binafsi, jamii zinazozunguka hifadhi zetu pamoja na sekta za fedha na usafirishaji hivyo jukumu la kudhibiti vitendo hivyo sio la kuiachia serikali pekee, lazima na sisi kama sekta binafsi tushiriki," alisema Victoria,

Alisema kwa kushirikiana na mashirika ya Uhifadhi ya TANAPA,TAWA, NCAA na TFS wametoa mafunzo kwa wadau wao ili kuhakikisha rasilimali hizo zinatumika kiutalii na kuongeza mchango katika pato la taifa kupitia sekta ya utalii.

Alisema katika kudhibiti uwindaji haramu, wamezishawishi sekta binafsi kutenga fedha maalum kwa ajili ya kusaidia wananchi waoishi pembezoni mwa hifadhi kufanya miradi mbalimbali ikiwamo ya kilimo, ufugaji na utengenezaji wa vitu vinavyovutia watalii badala ya kushiriki katika ujangili.

Mkurugenzi Mtendaji wa JET, John Chikomo, alisema mafunzo hayo kwa waandishi wa Habari yanakusudia kuibua changamoto zinazoikabili sekta ya utalii pamoja na kukomesha biashara ya usafirishaji wa wanyamapori pamoja na uwindaji haramu katika hifadhi mbalimbali zilizopo hapa nchini.

Chikomo aliwataka waandishi wa habari za uhifadhi na mazingira kutumia nafasi hiyo kupaza sauti zao na kutoa mchango kwa Serikali kwa ajili ya kusaidia kudhibiti vitendo vya ujangili ili kuvutia watalii kuja nchini ya kujionea vivutio vya utalii vilivyopo.

HABARI KITAIFA

## Pwani kuchanja polio watoto 200,000

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKOA wa Pwani unatarajia kutoa chanjo ya matone ya polio kwa watoto zaidi ya 200,000 wenye umri chini ya miaka mitano kuanzia Aprili 28 hadi Mei Mosi.

Mpango huo ulibainishwa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa chanjo Mkoa wa Pwani, Abas Hincha, katika kikao cha kamati ya msingi ya mkoa huo iliyokuwa inajadili kuhusiana na kampeni ya chanjo ya polio.

Hincha alisema chanjo hiyo itakuwa inatolewa nyumba kwa nyumba kwa watoto ambao hawajapata chanjo hiyo.

Alisema mwananchi ambaye ataona muda uliopangwa unapita na mtoto wake hajapata chanjo anatakiwa kufika kwenye vituo vya huduma ya afya.

Mganga Mkuu wa mkoa wa Pwani, Dk Gunini Kamba, aliwahimiza wananchi kutoa ushirikiano kwa waratibu watakaokuwa wanapita nyumba kwa nyumba ili kufanikisha kampeni hiyo.

"Chanjo hii ni salama kwa watoto na ni kwa ajili ya kuzuia ugonjwa wa polio kwa watoto chini ya miaka mitano, ambapo pia katika kampeni hiyo itaongeza uelewa kwa jamii kuhusiana na ugonjwa huo," alisema Dk. Gunini.

Akizungumza katika kikao hicho kwa niaba ya Mkuu wa mkoa wa Pwani, Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Martine Ntemo, alisema lengo la kampeni hiyo ni kuongeza kinga, kuzuia mlipuko na kudhibiti watoto wasipatwe na virusi vya ugonjwa huo.

Ntemo alitoa rai kwa kamati za afya ya msingi kuhakikisha wanashiriki kikamilifu kuhamasisha jamii wanapopita kwenye nyumba zao kufanikisha watoto wanaolengwa wanapata chanjo hiyo.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Musoma mkoani Mara juzi, ambayo inajengwa katika kitongoji cha Kwikonero, Kijiji cha Suguti jimbo la Musoma Vijijini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wataka mabinti kushika nafasi za uongozi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WANAHARAKATI wa kupambana na vitendo vya udhalilishaji na kuhamasisha wanawake kushika nafasi za uongozi wamewataka kina mama katika Kisiwa Cha Kojani Wilaya ya Wete kuwapa kipaumbele watoto wa kike katika kugombania nafasi za uongozi.

Wakizungumza na wanawake hao huko katika kisiwa hicho , wanaharakati hao walisema ni vyema kwa akina mama kuwashajihisha watoto wao wa kike kugombania nafasi mbalimbali za uongozi hata wakati wakiwa shule.

Mohammed Said kutoka jumuia ya PECAO alieleza kuwa kwa muda mrefu wanawake wamekuwa nyuma katika kushika nafasi za uongozi na hivyo kupelekea mambo yao mengi kutolewa uamuzi na wanaume.

Mohammed aliwataka wanawake hao kuwapa nafasi za uongozi wanawake wenzao ili wakatoe changamoto zao katika mabaraza ya kutunga sheria pamoja na sehemu mbalimbali ambazo watapata kutoa kero zao.

Aidha Mohammed alisema kuwa uongozi hauhitaji kusoma sana bali ni mtu mwenye kujielewa pamoja na kufanya uchambuzi sahihi kwa yale ambayo anayawakilisha kwa jamii husika.

Sambamba na hayo Mohammed alieleza kuwa kumekuwa na jumuia mbalimbali ambazo zimeanzishwa katika jamii lakini nafasi kubwa ambayo anapata mwanamke ni mshika fedha tu. "Tuondokane na ile dhana ya kuwa mwanamke hafai katika uongozi, hili sio kweli kwani hata dini imeruhusu mwanamke kuwa kiongozi,"alisema Mohammed.

Akizungumzia suala la udhalilishaji kwa wanawake na watoto, Mohammed alisema kuwa tatizo hilo lipo na limekuwa ni kero kwa serikali na wananchi kwa ujumla.

Aliwataka akina mama hao kurudisha malezi yaliyokuwepo hapo nyuma kwa kushirikiana pamoja.

"Lakini pia tuweze kufuatilia nyendo za watoto wetu kila wakati pamoja na kuchukua hatua zinazostahiki kwa wale ambao watapatikana na tuhuma za udhalilishaji, muhali sio mzuri tuacheni,"alisema Mohammed.

Nae Hamad Omar Khamis (PECAO) alisema kuwa lengo la mkutano huo ni kuwashajihisha wanawake kujiingiza katika mfumo wa uongozi. Alieleza kuwa ukifuatilia kwa umakini zaidi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar wengi waliomo kule ni wanaume.

"Mbali na kutoa elimu kwa kina mama juu ya uongozi lakini pia tumekuwa tukisikiliza changamoto ambazo mnakabiliana nazo katika maeneo yenu ili tuweze kuzitafutia ufumbuzi,"alieleza Hamad.

Nae Mhamasishaji Raya Said Ali, aliwataka kina mama hao kujiunga katika vikundi vya wajasiriamali ili waweze kujikomboa na umasikini.

Alieleza kuwa Serikali imetenga fedha nyingi kwa ajili ya kusaidia vikundi vya wajasiriamali, hivyo aliwataka kujikusanya pamoja na kuunda vikundi vyao.

Nao akina mama hao walisema kuwa changamoto kubwa ambayo ipo katika Kisiwa Cha Kojani ni wanawake wengi ambao wanaishi huko hawajui kusoma wala kuandika na hivyo kupelekea ugumu katika mambo ya uongozi

Mbali hiyo walieleza changamoto nyengine kuwa ni uhaba wa madaktari wa kike ambao wanazalisha katika Kituo cha Afya cha Kojani kuwa ni kidogo sana.

"Lakini pia kwa upande wa huduma za kijamii tumekuwa na upungufu wa madaktari wa kuzalisha katika kituo chetu cha afya pamoja na madawa, pia tuna upungufu wa walimu katika Skuli yetu ya Msingi Kojani, hivyo tunaiomba serikali kutupatia ajira za walimu kwani wapo vijana ambao wameshasomea na wanajitolea katika skuli yetu," walisema akina mama hao.

Mkutano huo umeandaliwa na jumuia zisizo za kiserikali za TAMWA, PECAO na ZAFELA ili kuwashajihisha wanawake waweze kujiingiza katika nafasi za uongozi.

## Wazalishaji mbegu wapata uhakika soko

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

Wazalishaji wa mbegu kutoka Tanzania sasa watakuwa na uhakika wa kuuza katika soko la ndani na nje ya nchi.

Uhakika huo unatokana na Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu (TOSCI) kujiunga na Skimu ya mbegu ya Shirika la Kimataifa linalotambua ubora wa mbegu katika nchi mbalimbali. Uhakika mwingine kwa wazalishaji hao kuuza mbegu zao kwenye nchi yoyote unatokana na TOSCI pia kuwa mwanachama wa Taasisi ya Kimataifa ya Hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea(UPOV) huku ikiwa na Hati ya Ithibati ya Kimataifa.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI, Patrick Ngwediagi, alisema hatua ya kutambuliwa na taasisi hizo za kimataifa inatokana na kusimamia katika kudhibiti ubora wa mbegu kitaifa na kimataifa.

" Sio nchi zote zinaweza kutambulika na taasisi hizo, mpaka ufikie viwango vya kimataifa sasa kutokana na kudhibiti ubora wa mbegu kitaifa na kimataifa tumeweza kufika hivyo vigezo na sasa tutauza kwenye nchi yoyote ile," alisema.

Alisema mafanikio ya kudhibiti ubora wa mbegu kitaifa na kimataifa yanatokana na ongezeko la mbegu zilizothibitishwa ubora katika kipindi cha mwaka 2014 /15 -2019/2020.

Alisema katika kipindi hicho,TOSCI ilizifanyia majaribio ya aina mpya za mbegu, kukagua mashamba, kufanya majaribio ya sampuli na kufanya vipimo kwenye mbegu zilizozalishwa ili kuhakiki ubora wake.

Kuhusu changamoto ya tatizo la mbegu feki na dhaifu zilizokuwa zikiuzwa kwa wakulima nchini na kuwasababishia hasara, Mkurugenzi huyo mkuu wa TOSCI alisema sasa limedhibitiwa kwa asilimia kubwa kutokana na kuongeza kasi ya matumizi ya lebo zake zenye ubora katika mbegu zinazozalishwa.

Alisema katika kipindi cha mwaka 2014/2015 matukio ya mbegu feki na dhaifu yalikuwa kati ya 300 mpaka 350, hivyo kuwasababishia hasara wakulima nchini na kuweka mikakati ya kudhibiti. Alisema kutokana na udhibiti wa mbegu feki, sasa wakulima wamekuwa na uhakika wa kupata mavuno kulingana na walivyopanda hatua ambayo imelisaidia Taifa kukuza uchumi wake.

"Ongezeko la matumizi ya lebo zetu zimeweza kulisaidia Taifa kuhakikisha mbegu zinazozalishwa na kupelekwa kwa wakulima zinakuwa na ubora unaotakiwa," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Uzalishaji wa mbegu ya Aminata, Dk Zubeda Mduruma, alisema tatizo kubwa lilikuwa ni soko, hivyo kutokana na TOSCI kukubalika kimataifa sasa watakuwa na uhakika wa kuuza mbegu hizo nje ya nchi.

Mwenyekiti wa Chama cha wakulima wa Alizeti Tanzania, Stephen Marealle, alisema uzalishaji wa mbegu unaotokana na Makampuni mbalimbali uende sambamba na ujenzi wa maghala ya kuhifadhi ili kuwafikia wakulima kwa wakati.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ameshaagiza taasisi za Serikali zinazotafiti, kuzalisha na kudhibiti mbegu kukaa pamoja na ili kujipanga kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora zitakazotosheleza wakulima na nyingine kuuzwa katika nchi za Afrika ikiwa mojawapo ya mikakati ya Serikali kuteka soko la mbegu bora nje ya nchi.

# Vijana waaswa kukimbilia mjini

**Na Sabato Kasika**

VIJANA wametakiwa kuacha mtindo wa kukimbilia mijini kufanya biashara ndogo, badala yake watumie fursa za kiuchumi zilizopo vijijini zikiwamo za kilimo, ufugaji, kuanzisha duka, ili kujiletea maendeleo.

Rai hiyo ilitolewa na Ofisa Miradi wa Asasi ya Kuunganisha Vijana Kimaendeleo Ruangwa (AKUVIKIRU), mkoani Lindi, Simon Ndallu, alipokuwa akizungumza na gazeti hili jana.

Ofisa Miradi huyo alisema, kwa sasa vijijini kuna fursa nyingi za kilimo na biashara nyingi, na kwamba karibu vijiji vyote nchini vina huduma ya umeme, ambayo kijana anaweza kubuni biashara ya kufanya kupitia nishati hiyo.

Alisema, pamoja na malalamiko ya baadhi ya vijana kuhusu ubovu wa miundombinu ya vijijini anaamini kuwa kwa sasa maeneo mengi vijijini yana kila aina ya miundombinu ya kuwawezesha kuendesha maisha yao.

"Inaumiza kuona vijana wakikimbilia mijini na kujikuta wakifanya biashara ambayo haiakisi maendeleo yao ya baadaye huku wakiacha fursa nyingi vijijini, ni vyema wakaachana na mtindo huo," alisema Ndallu.

Alisema, kijana anaweza kuwa na mashamba ya muhogo au mazao mengine ya biashara ambayo yana soko kubwa nje ya nchi na kujipatia mtaji wa kutosha kupanua biashara badala kuhangaika na umachinga.

"Kwa mfano, muhogo una soko kubwa China, hiyo ni nafasi nzuri ya kuchangamkia kuliko kukimbilia mijini kuuza pipi, biskuti, karanga na vitu vingine vidogo ambavyo haviwezi kumnyanyua kiuchumi," alisema.

Alisema, vijijini kuna biashara nyingi ikiwamo kuuza mazao ya vyakula yatokanayo na kilimo au ufugaji, ambapo kijana anaweza kununua mazao wakati wa msimu wa mavuno na kuhifadhi.

"Wakati wa uhaba wa chakula anaweza kuuza kwa bei ya juu, lakini pia kijana anaweza kufungua duka akawa anakwenda mjini kununua bidhaa na kuiuza kwa bei ya rejareja au jumla," alisema.

Alisema, cha kushangaza, baadhi ya vijana wamekuwa wakitoa sababu za kukimbilia mijini kuwa ni kutokana na hali ngumu ya maisha na ukosefu wa miundombinu ya kuwawezesha kumudu maisha ya vijijini.

Ndallu alisema, anaamini kuwa binadamu aliyekamilika ni lazima atakuwa na fikra za namna gani anaweza kujikwamua na kutengeneza fedha ili maisha yake yawe mazuri, na kwamba hakuna anayependa kuishi maisha ya mateso.

Alisema, umefika wakati kwa kila kijina kujiuliza kama kweli fursa zote za kiuchumi ziko mijinin tu? Anaongeza kuwa jibu ni kwamba si kweli bali iwe mjini au vijijini, fursa za kiuchumi zipo kote. Katika ufafanuzi wake, alisema, hata mijini kuna changamoto zake, na kwamba wapo baadhi ya watu waishio huko wanakula mlo mmoja kwa siku, kutokana na ugumu wa maisha, na kwamba ni muhimu vijana kutafakari hilo.

"Lakini pia wapo baadhi ya vijana wanaokimbilia mijini kufanya biashara na kuishia kulala kwenye mitaro, vituo vya mabasi au kujiingiza katika vitendo viovu na kuishia kwenye mikono ya dola," alisema.

Kiongozi huyo alisema, kijana mwenye nguvu za kuzalisha mali kuishi mjini bila kuwa na kitu cha maana kinachomwingizia fedha, siyo ujanja, na kwamba ni vyema kijana kutazama kwa upana fursa zinazoweza kupatikana hata vijijini.

# Polisi Pemba kudhibiti wizi mifugo

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

JESHI la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba limesema, utaratibu walitakaoutumia kwa sasa ni kufanya doria katika maeneo ya mabondeni, ili kudhibiti wizi wa mifugo katika mkoa huo.

Akizungumza na mwandishi wa habari Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba, Juma Khamis, alisema wizi wa ng'ombe umekuwa ni tatizo kubwa katika mkoa huo ambalo linaathiri jamii.

Alisema kuwa, licha ya elimu wanayoitoa kwa wafugaji na wananchi kuhusu ufugaji wa ng'ombe katika maeneo salama lakini bado haijafuatwa, jambo ambalo linawarahisishia wezi kuchukua mifugo hiyo bila ya woga.

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi sasa limejipanga kufanya msako katika maeneo ya mabondeni na iwapo watakuta ng'ombe hayupo maeneo salama watamchukua na kumpeleka kwenye zizi la serikali ili kuepuka wizi wa mara kwa mara.

"Tunatoa elimu sana kwa jamii kwamba, wafugaji wajikusanye pamoja na watengeneze sehemu yao maalumu ya kuweka mifugo yao lakini wanakataa, hiyo inasababisha ng'ombe hao kuibiwa", alisema Kamanda huyo.

Alisema miaka ya sasa ni tofauti na ya zamani kwa kuwa imani za watu zimebadilika, hivyo ni vigumu kulaza mifugo mahala popote.

"Jamii ya sasa imeharibika, vijana wanaiba mchana kweupe na wala hawaogopi, hivyo ili kuepusha kuibiwa mifugo yetu, tuiweke sehemu salama," alisema.

Vilevile alieleza kuwa, tatizo la wizi wa ng'ombe katika mkoa huo limekuwa kubwa, ambapo juzi waliibiwa ng'ombe wawili katika shehia ya Bopwe Wilaya ya Wete. Sambamba na hilo, Kamanda Sadi alisema wataendelea kupambana na wale wote wanaojihusisha na vitendo vya wizi na kuwachukulia hatua stahiki.

"Hatua kali za kisheria tutazichukua kwa yeyote anaejihusisha na wizi, kwa sababu wanadumaza maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla", alieleza.

Katika miezi miwili iliyopita ng'ombe takribani nane wameshaibiwa katika mkoa huo hivyo kuwatia hasara wafugaji wa maeneo hayo.



Baadhi ya waumini wa Kiislamu wakimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Stanbic Tanzania, Kevin Wingfieldm alipokuwa akizungumza nao wakati wa hafla ya iftar iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake jijini Dar es Salaam juzi. Hafla hiyo ilihudhuriwa na Mufti wa Tanzania, Shekhe Aboubakary Zubeiry, viongozi wengine wa ngazi ya juu kutoka Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) na wadau mbalimbali wa benki hiyo wakiwemo wateja na wafanyakazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu soko duni bidhaa za Tanzania hizi

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Viwanda Vidogo (SIDO), limebaini kwamba sababu ambazo zinachangia soko duni ndani na nje ya nchi kwa bidhaa za Tanzania, ni kutokidhi hadhi ya ufungashaji na namna ya kuielezea bidhaa sokoni.

Limesema bidhaa yoyote na bei yake sokoni hutegemea namna ilivyo fungashwa, maelezo na mwonekano mzuri na yenye mvuto, kukabiliana na ushindani uliopo sokoni.

Msimamizi wa Kituo cha Ufungashaji SIDO Dar es Salaam, Antonia Masoy, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, akiwasilisha mada iliyolenga kuwapa mbinu wajasiriamali wa bidhaa za kufungasha na wenye viwanda vya kuzalisha vifungashio, ili kuteka soko;

Mkutano uliwakutanisha wajasiriamali wa ufungashaji bidhaa pamoja na wazalishaji wa viwanda vya vifungashio kujadili fursa na changamoto zilizoko kwenye ufungashaji, kuzitambulisha na kukuza nembo.

Alisema kabla ya mkutano huo utafiti uliofanywa na idara yake eneo la soko kuu Kariakoo, jijini Dar es Salaam, ulibaini wafanyabiashara wengi wanaouza bidhaa za kufungasha huagiza vifungashio nchi jirani.

"Bidhaa yeyote na bei yake sokoni inategemea namna ilivyo na mwonekano mzuri na yenye mvuto sokoni. Kifungashio kinachovutia baadhi hudhani bidhaa imetoka nje, ukizungumza na wafanyabiashara, wajasiriamali kwa nini wananunua vifungashio nje, wanatuambia vya Tanzania sio imara, vinavunjika, vinafubaa mapema kwenye 'shelf' kabla bidhaa haijanunuliwa," alisema Antonia.

Alisema shirika hilo litaandaa mtandao ambao utawezesha kuwakutanisha wajasiriamali wa bidhaa za kufungasha na wenye viwanda vya vifungashio nchini, na kwa kuanzia wamewakutanisha kutoka Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam, ili kuongeza ubora wa bidhaa na kukuza soko la ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi wa Masoko na Uwekezaji wa SIDO, Shoma Kibende alisema shirika hilo limebaini kuna changamoto kubwa katika namna ya kufanya ufungashaji na nembo kuelezea bidhaa na kusababisha bidhaa za Kitanzania kupata ushindani duni sokoni.

"Kinachoondoa mvuto wa bidhaa sokoni ni pamoja na namna ya kuzi-brand, kuna changamoto ya vifungashio kwa wajasiriamali kwa sababu vipo vinavyofanana sokoni na kumchanganya mteja. Hii inatokana na uchache au uhaba wa upatikanaji vifungashio sahihi mahali alipo mjasiriamali," alisema Kibende.

Kibende alisema mkoani Dar es Salaam kuna mahitaji ya vifungashio kutokana na uchache wa viwanda vya kutengeneza vifungashio vinavyokidhi ushindani wa soko.

"Natoa wito kwa wajasiriamali kuitumia SIDO kupata vifungashio vizuri. Leo tumewaita wenye viwanda 11 kutoka mkoani Pwani na Dar es Salaam ili wabainishe tatizo lilipo na kupata ufumbuzi, ingawa mkakati wetu ni kufikia malengo na kuuza bidhaa hata nje, ikiwa bado inavutia," alisema Kibende.

Kaimu Meneja Mkuu kutoka kampuni ya Nampack Tanzania, Benjamin Mutua, alisema kampuni hiyo inajihusisha na kutengeneza vifungashio vya chuma ikiwamo makopo kwa ajili ya kuhifadhi vyakula kama vile korosho na nyinginezo zinazosindikwa.

Mutua alisema hivi sasa wamesitisha kutoa huduma ya vifungashio hivyo kutokana na ushindani mkubwa sokoni na kwamba wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa kama hiyo nje ya nchi huuza kwa bei ndogo kuliko wao, akisema kampuni hiyo huagiza malighafi nje ya nchi ili kuandaa vifungashio vya chuma.

"Vifungashio vya chuma ni bora na imara, lakini sasa tunakabiliwa na ushindani sokoni na tumeacha kuzalisha. Uzalishaji wetu ulisaidia wajasiriamali wa bidhaa za pombe kuwatengenezea vizibo vya chuma kwa bei nzuri," alisema Mutua.

Nipashe
Spotika



REKODI 11 ZA EPL AMBAZO HAZITAVUNJWA HIVI KARIBUNI UK. 12-13



SALAH

# SABABU 3 LIVER WAMUONGEZEA MKATABA SALAH, 2 ASIONGEZWE

**LIVERPOOL,** England

MHOAMED Salah kwa sasa ndiye mchezaji muhimu zaidi katika klabu ya Liverpool huku akitarajia kushinda mataji matatu mwaka huu. Mmisri huyo amethibitisha ubora wake mara kwa mara na ametoa sababu za kutosha kutoa hoja ya kuchukuliwa kama mchezaji wao mkuu.

Lakini mkataba wa winga huyo unatarajiwa kufikia tamati mwaka ujao na mazungumzo ya mkataba yameripotiwa kukwama kati ya pande hizo mbili.

Kinyume na hapo, faida za kurefusha mkataba wa nyota huyo wa Kiafrika zinazidi hasara yake. Lakini hoja ya haki inaweza kufanywa kwa kesi zote mbili. Ingawa kumpoteza kwa uhamisho wa bure msimu ujao inaweza kuwa hali bora ya Liverpool, na pia inaweza kuwa mbaya.

Hebu tuangalie kwanza sababu kwa nini Liverpool imuongezee mkataba Salah. Hapa kuna sababu tatu kwa nini Liverpool wanapaswa kuchukua uamuzi huo...

### #1. UHAKIKA WA MABAO 15 KWA MSIMU

Liverpool imekuwa na historia ya wafungaji bora kama Michael Owen, Robbie Fowler, Fernando Torres na Luis Suarez. Lakini wachache wametoa uthabiti ambao Salah ameuonesha kwa miaka mitano iliyopita.

Ingawa Mmisri huyo hajafunga katika mechi tatu zilizopita za Ligi Kuu, ana mabao 20 na asisti 11 kwenye ligi msimu huu. Kwa hakika, amefunga zaidi ya mabao 15 ya ligi katika kila msimu mmoja kati ya misimu yake mitano. Ili kuweka mambo sawa, hakuna mchezaji mwingine wa Ligi Kuu ambaye ameweza kufanya hivyo.

Kwa hiyo, kumpoteza mchezaji ambaye anaweza kutoa mabao mara kwa mara kunaweza kuwa hatari kwa Liverpool. Hivyo ni muhimu wamuongezee mkataba wake haraka iwezekanavyo.

### #2. REKODI, UTIMAMU WA MWILI

Salah anafikisha umri wa miaka 30, mwaka huu, lakini utimamu wake wa mwili unaendelea kuwa sawa, sifa muhimu kwa Liverpool kumpa mkataba mpya.

Katika misimu mitano iliyopita, Salah amecheza mechi 174 kati ya 183. Pia amekuwa sehemu muhimu ya kila mashindano yao. Mengi haya yanatokana na mfumo wa utimamu wa winga huyo na viwango vyake vya stamina.

"Amefanyia kazi mwili wake, ni mwili wake, lakini ni wazi hakuna miujiza. Wachezaji wako hatarini zaidi kuliko wengine na Mo ana mawazo sahihi, mtazamo sahihi na mwili sahihi pia," kauli ya kocha wake, Jurgen Klopp.

### #3. NI MCHEZAJI WA MECHI KUBWA

Moja ya sababu kuu za mafanikio ya Liverpool chini ya Jurgen Klopp ni uchezaji wao kwenye mechi kubwa. Matokeo yao dhidi ya timu sita bora za Ligi Kuu England, pamoja na klabu nyingine kubwa Ulaya, yamewafanya kushinda mataji mengi.

Lakini matokeo haya yamewezekana kutokana na rekodi ya Salah ya kufunga mabao dhidi yao. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29, amekuwa na mchango wa mabao 35 katika mechi 47 za Ligi Kuu dhidi ya timu sita bora katika kampeni tano zilizopita. Wakati huo huo, pia amefunga katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya 2019 dhidi ya Tottenham Hotspur.

Salah sasa amehusika moja kwa moja katika mabao 35 katika mechi 47 za Ligi Kuu dhidi ya 'timu kubwa sita' akiwa na Liverpool. Winga huyo huwa anajitokeza wakati wa mechi kubwa na hufanya kama mleta tofauti kwa Liverpool. Ikiwa wataongeza mkataba wake, hii itakuwa sababu kubwa ambayo itazingatiwa.

Sasa kwa kuwa tumeona sababu za Liverpool kurefusha mkataba wake, tuangalie upande wa pili. Hizi ndizo sababu mbili kwa nini Salah hapaswi kukabidhiwa mkataba mpya Liverpool.

### 1#. MKATABA MKUBWA UTAVURUGA MISHAHARA, MTAFARUKU KIKOSINI

Iwapo Liverpool itaamua kumuongezea mkataba Salah, inaweza kusababisha matatizo kuhusu bajeti yao.

Salah ni mchezaji anayestahili kubaki, lakini 'Wekundu' hao watalazimika kutoa fedha nyingi. Wamiliki wa klabu hiyo, FSG wako tayari kumuongezea mkataba wake wa kulipwa pauni 300 kwa wiki au zaidi. Lakini wanaripotiwa kutoweza kufikia makubaliano ya kumlipa pauni 400 kwa wiki ambazo wawakilishi wa mchezaji huyo wanataka.

Cristiano Ronaldo, Kevin de Bruyne, na wengine kadhaa wanaripotiwa kupata zaidi ya pauni 400 kwa wiki. Kwa hiyo, Mmisri haombi chochote kisicho cha kawaida.

Lakini kumpa winga huyo dili kubwa kama hilo kunaweza kuvuruga mpangilio wa mishahara hapo Anfield na kusababisha nyota wengine kuulizia nyongeza ya mishahara yao.

Muundo wa mishahara ulioimarishwa umekuwa ufunguo wa mafanikio ya klabu chini ya FSG na kuvunjwa kwa mchezaji yeyote kunaweza kuwaweka kwenye wakati mgumu.

### 2#. WANAWEZA KUSAJILI VIPAJI VIPYA

Ingawa kumekuwa hakuna dalili kwamba washindi hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka jana, wanataka kumbakiza Salah, kuna uwezekano wa kweli. Iwapo mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri ataamua kutosaini mkataba mpya msimu huu wa majira ya joto, wanaweza kumuuza kwa faida badala ya kumpoteza bure mwishoni mwa mkataba wake.

Wangeweza kutumia fedha hizo kusajili vipaji chipukizi, jambo ambalo mfumo wao wa skauti umefanya vema kwa miaka mingi. Kuongezwa kwa Luis Diaz na Diogo Jota, pamoja na kuwakuza Harvey Elliot na Curtis Jones, kumekuwa mfano mzuri.

Kwa kuzingatia kuongezeka kwa hisa za mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, katika soka la Ulaya, klabu nyingi zitataka kumsajili msimu wa majira ya joto na klabu hiyo ya Anfield inaweza kumuuza kwa fedha nyingi.

## ISIKUPITE

WAKATI Bayern Munich ikifanikiwa kutwaa taji la 10 mfululizo la Bundesliga baada ya kuifunga Borussia Dortmund mabao 3-1 juzi, mshambulizi wa mabingwa hao, Thomas Muller, amekuwa mchezaji wa kwanza kushinda mataji 11 ya Bundesliga.



## Extra Time

# REKODI 11 ZA EPL AMBAZO HAZITAVUNJWA HIVI KARIBUNI


ARSENE WENGER

**LONDON,** England

LIGI Kuu ya England (EPL), inachukuliwa kuwa moja ya ligi za mpira wa miguu zenye ushindani zaidi ulimwenguni. Tangu ilipoundwa upya mwaka 1992, imepata umaarufu mkubwa.

**Hapa tunaangalia baadhi ya rekodi za mtu binafsi na za timu ambazo zimewekwa ambazo haziwezi kuvunjwa au kufikiwa hivi karibuni, twende sasa...**

### #1. Mechi nyingi mfululizo bila kupoteza: Arsenal - 49

Huko nyuma mwaka 2002, kocha wa Arsenal, Arsene Wenger, alisema (imeripotiwa kuwa nilinukuliwa vibaya), “Bado nina matumaini tunaweza kuvuka msimu bila kupoteza mchezo, waandishi wa habari na mashabiki wa wapinzani walimdhihaki.”

Lakini Wenger aliishi kulingana na kauli hiyo, kwani ‘Washikabunduki’ hao walishinda msimu wa 2003/04 kwa raha - bila kupoteza mchezo. Rekodi yao ya msimu huo ilisomeka (Mechi 38, kushinda 26, sare 12, kupoteza 0), wakishinda taji mbele ya washindi wa pili Chelsea kwa tofauti ya pointi 11. Kikosi hicho kiliingia kwenye historia na kuitwa kama ‘The Invincibles’.

Nini zaidi; walikwenda kuvunja rekodi ya michezo mingi bila kupoteza iliyowekwa na Nottingham Forest (michezo 42). Mbio hizo zilifikia kikomo baada ya kufungwa mabao 2-0 na Manchester United kwenye Uwanja wa Old Trafford.

### #2. Mabao mengi ya mchezaji aliyetokea bechi mchezo mmoja: Ole Gunnar Solskjaer - 4

Wakati Manchester United ilipocheza na Nottingham Forest msimu wa 1998/99, kilichojiri kitakumbukwa kwa zaidi ya ukweli kwamba, mechi hiyo ilichezwa katika kumbukumbu ya maafa ya ndege ya Munich.

Ingawa matokeo yalikuwa sawa ndani ya dakika saba bao 1-1, ‘Mashetani Wekundu’ hao walienda kushinda 1-8. Paul Scholes, Andy Cole na Dwight Yorke waliirarua Nottingham Forest katika kipindi cha kwanza na cha pili. Na Solskjaer hakuingia uwanjani hadi dakika ya 72 ya mchezo.

Mshambuliaji huyo wa Norway alifunga bao lake la kwanza katika dakika ya 80, la pili dakika ya 88 alipomzunguka kipa, alifunga la tatu ‘hat-trick’ dakika chache baadaye Paul Scholes kumlisha pasi. Bao lake la nne lilikuja dakika za majeruhi.

Baada ya mchezo huo, Solskjaer alikiri kwamba alidhani hatawahi kupata nafasi ya kucheza wakati United ikiongoza 4-1, lakini Sir Alex Ferguson alimpa nafasi.

### #3. Pointi nyingi msimu mmoja: Chelsea - 95

Msimu wa 2004/05, ulikuwa mpambano wa karibu kwa kipindi kirefu cha msimu, huku Arsenal (mabingwa watetezi), Manchester United na Chelsea wakiwa kwenye mbio moja.

Lakini Arsenal walipoteza mvuto baada ya kufungwa na Man United kwenye Uwanja wa Old Trafford (mchezo uliomaliza mbio zao za kutopoteza mechi).

Lakini ni ‘The Special One’ Jose Mourinho aliyeiongoza Chelsea kutwaa taji lao la kwanza kabisa la Ligi Kuu, nusura awaige wapinzani wao wa London kwa kukaa msimu mzima bila kufungwa. Rekodi yao ya mwisho ilikuwa (mechi 38, ushindi 29, sare 8, kupoteza mechi moja - pointi 95 na mabao 57.

Frank Lampard alikuwa mfungaji bora wa klabu hiyo akiwa na mabao 13, akifuatiwa na Eidur Gudjohnsen mwenye mabao 12. Chelsea pia walikuwa wameshinda Kombe la Ligi baada ya kuishinda Liverpool msimu huo.

### #4. Mabao mengi ya Ligi Kuu: Alan Shearer - 260

Kati ya mwaka 1992 na 2006, jumla ya mechi 441 za Blackburn Rovers (1992-1996) na Newcastle United (1996-2006), Shearer alifunga mabao 260.

Shearer aliiongoza Blackburn Rovers kunyakua taji la Ligi Kuu msimu wa 1994/95, akifunga rekodi ya pamoja ya EPL mabao 34 msimu huo. Na mwaka 1996, alifanya uhamisho wa rekodi ya dunia wakati huo kwenda klabu ya nyumbani kwao Newcastle United kwa ada ya pauni milioni 15. Mshambuliaji huyo alijijengea jina katika klabu hiyo na akaendelea kuichezea kwa muongo mmoja, akifunga mabao na kuvunja rekodi katika mchakato huo. Alikuwa amefunga mabao 206 katika mashindano yote kwenye mechi 395 pekee akiwa na Newcastle hadi alipostaafu mwaka 2006.

### #5. Bao la umbali mrefu zaidi: Tim Howard mita 93

Ndiyo, sote tumeona magolikipa wakifunga mabao - penalti, mipira ya adhabu, mipira ya kichwa kutokana na kona. Lakini ni mara ngapi unaona kipa akifunga kutoka kwenye sanduku lake?

Hivyo ndivyo Howard alivyofanya wakati Everton ilipocheza na Bolton Wanderers pale kwenye Uwanja wa Goodison Park.

### #6. Mchezaji aliyezifungia klabu nyingi zaidi: Craig Bellamy - 7

Mshambuliaji huyo wa Wales alianza uchezaji wake wa ngazi ya juu katika madaraja ya chini akiwa na Norwich City, lakini hakucheza Ligi Kuu England hadi mwaka 2000 akiwa na Coventry City.

Kisha angeenda kuchezea Newcastle (2001-2005), Blackburn Rovers (2005-2006), Liverpool (mara mbili kati ya 2006-2007 na 2011-2012), West Ham United (2007-2009), Manchester City (2009- 2011) na Cardiff City (mara mbili wakati wa 2010-2011 kwa mkopo na 2012-2014).

Alistaafu akiwa na klabu hiyo ya Wales akiwa amefunga jumla ya mabao 81 kwenye mechi 294 katika klabu saba tofauti.

### #7. Hat-trick ya haraka zaidi: Robbie Fowler - dakika 4 sekunde 33

Mshambulizi wa Liverpool, Robbie Fowler aliwahi kufunga mabao matatu ‘hat-trick’ katika muda wa chini ya dakika tano na timu aliyoifunga haikuwa iliyopo kwenye tishio la kushuka daraja, bali ni Arsenal.

Katika mchezo wa awali wa Anfield Agosti 28, mwaka 1994, Fowler alifunga mabao matatu ndani ya sekunde 273 na kuwapa ‘Wekundu’ hao uongozi wa mabao 3-0.

### #8. Mechi nyingi zaidi: Ryan Giggs - 632

Hadi msimu wa 2013/14, Ryan Giggs alishikilia rekodi kadhaa. Mojawapo ilikuwa mechi nyingi zaidi katika Ligi Kuu England kuwahi kutokea - michezo 632.

Mchezaji huyo wa Wales amekuwa sehemu ya Ligi Kuu ya England tangu ilipoanzishwa upya mwaka 1992 na alistaafu Mei 2014 akiwa na umri wa miaka 40, jambo ambalo linazungumza mengi kuhusu utimamu wake na kujituma kwa mchezo huo.

### #9. Mechi nyingi mfululizo nyumbani bila kupoteza: Chelsea - 86

Yote yalianza Februari 21, 2004 wakati Chelsea ya Jose Mourinho ilipofungwa mabao 1-2 pale Stamford Bridge na wapinzani wa London, Arsenal. Walishinda mchezo wao uliofuata wa nyumbani Machi 20, 2004 dhidi ya Fulham.

Hawakupoteza mchezo wa nyumbani hadi Liverpool walipotembelea Stamford Bridge Oktoba 26, 2008. Chelsea walipoteza kwa Liverpool shukrani kwa bao pekee kutoka kwa Xabi Alonso.

### #10. Bao la haraka zaidi la mchezaji kutoka benchi: Nicklas Bendtner - sekunde 1.8

Nani angefikiria kwamba Nicklas Bendtner wa Arsenal angepata nafasi katika historia?

Mshambuliaji huyo, ambaye alikuwa maarufu zaidi kwa uchezaji wake wa nje ya uwanja kuliko ushujaa wake wa uwanjani, anashikilia rekodi ya kufunga bao la haraka zaidi kwa mchezaji wa akiba - sekunde 1.8.

Kwa kuongezea, lilikuwa pia bao lake la kwanza kwa Arsenal kwenye Ligi Kuu.

Bao lenyewe lilikuwa la daraja la juu. Akiwa ameingia kuchukua nafasi ya Emmanuel Eboue wakati Arsenal ilipopata mpira wa kona, alipaa juu ya safu ya ulinzi ya Tottenham na kuunganisha kwa kichwa kona ya Cesc Fabregas.

### #11. Ushindi mara chache kwa msimu: Derby County - ushindi 1

Derby County ilikuwa na msimu mbaya 2007/08. Na hilo litakuwa ni jambo lisilosahaulika.

Baada ya kupandishwa daraja hadi EPL, mashabiki wao walikuwa na shauku kubwa. Lakini mambo yalikuwa tofauti baada ya kushinda mchezo mmoja tu kwa bao 1-0 dhidi ya Newcastle huku Kenny Miller akifunga kwenye mechi yake ya kwanza.

Lakini rekodi yao ya mwisho ilisoma (mechi 38, ushindi 1, sare 8, kupoteza 29). Walikuwa wamefunga mabao 20 pekee katika mechi 38, na kuruhusu mabao 89 katika mchakato huo. Walishushwa daraja baada ya msimu mmoja tu kwenye Ligi Kuu.


Nahodha wa zamani wa Arsenal, Patrick Vieira akinyanyua kombe baada ya kukabidhiwa kwa kulitwaa msimu wa 2003/04 bila kupoteza mechi. Kushoto ni aliyekuwa kocha wa timu hiyo, Arsene Wenger.
**PICHA: MTANDAO**

## Nukuu

“Nilidhani kwamba Gabi (Martinelli) angepiga, nilipoona kwamba Bukayo (Saka) aliichukua, kwa uaminifu, jambo langu la kwanza ambalo nilifikiria lilikuwa nyuma katika msimu wa majira ya joto na kile kilichotokea. Kwa yeye kuwa na ujasiri wa kusema ‘nitaichukua tena’ kwa sababu nina hakika ilikuwa nyuma ya akili yake, kwangu ni jambo jema kwake,” **Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta akimsifu Bukayo Saka baada ya kufunga penalti yake ya kwanza (dhidi ya Chelsea) tangu alipokosa kwenye fainali ya Euro 2020 akiwa na kikosi cha England.**



“Ni heshima kubwa kuteuliwa kuwa kocha wa Manchester United na nimefurahishwa sana na changamoto iliyo mbele yangu. Naijua historia ya klabu hii kubwa na shauku ya mashabiki, na nimedhamiria kabisa kuendeleza timu yenye uwezo wa kuleta mafanikio yanayostahili,” **Kocha ajaye wa Manchester United, Erik ten Hag.**



“Hapana, haijaisha, lakini iko karibu sana. Kila mtu anasubiri kushindwa kwa Real Madrid, lakini bado tupo nguvu kubwa. Historia ya klabu hii, ubora wa wachezaji na hisia zao za kuhusishwa, wanahisi kitu cha pekee wanapovaa jezi za timu hii. Sio jambo jipya kwa Real Madrid na nadhani hii ndiyo sababu,” **Kocha wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, akikiri kuwa wanakaribia kutwaa ubingwa wa LaLiga.**





Vinara wa Ligi Kuu Tanzania, Yanga ambao wanashikilia rekodi ya kushinda mechi nyingi, magoli mengi, huku ikiwa haijapoteza mechi hata moja msimu huu. **PICHA: MAKTABA**

# LIGI KUU BARA KATIKA NAMBA

**Na Adam Fungamwango**

KWA sasa Ligi Kuu Tanzania Bara inaelekea ukingoni, huku Yanga ikionekana imedhamiria msimu huu kutwaa ubingwa huo kwa mara ya kwanza baada ya misimu minne.

**Hii inachagizwa na ushindi wa mabao 2-1, iliyoupata Jumamosi iliyopita dhidi ya Namungo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kuiweka kwenye sehemu nzuri zaidi ya kufanikisha ndoto hizo.**

Ukweli ni kwamba kimahesabu Yanga bado huwezi kuipa ubingwa, lakini kiuhalisia iko karibu mno na ubingwa wenyewe.

Hata wafuasi wa Simba, wanalijua hilo, ndiyo maana Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amekuwa akikiri kwenye vyombo vya habari kuwa wanapambana kwa ajili ya kuwafukuza watani zao wa jadi, lakini ni ngumu kutokana na tofauti kubwa ya pointi, kwani wao wanaweza kushinda mechi zote, lakini hawana uhakika kama wenzao watapoteza lini.

Hata hivyo, hii inachagizwa zaidi na kwamba tayari Simba ina tiketi mkononi ya kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao, iliyopatikana baada ya kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuitwanga US Gendamarie ya Niger mabao 4-0, hivyo kuonekana kupunguza nguvu za kuusaka ubingwa, kwani msimu ujao nchi itapeleka timu nne na wao wakiwamo.

Ni kwa sababu inaonekana nayo imejiwekea ufalme wake kwenye nafasi ya pili inayoonekana ni ngumu kufikiwa na timu zingine, si kimahesabu, bali kiuhalisia.

Wakati suala la ubingwa likionekana ni kama limekwisha, kumekuwa na vita ya kutafuta mshindi tatu, huku timu za Namungo, Azam na Geita Gold zikionekana kupambana kuipata, kwa sababu itaiwezesha moja ya timu hiyo kucheza kimataifa msimu ujao.

Katika tunakuletea takwimu, rekodi na msimamo wa Ligi Kuu kwa mtindo wa namba wakati huu ikielekea ukingoni...

**54 -** Ni pointi za vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga ambazo ni nyingi zaidi kuliko timu nyingine yoyote.

**41 -** Simba inamiliki idadi hii ya pointi kwenye kibindo chake mpaka sasa ikiendea kuweka namba kwenye nafasi ya pili.

**35 -** Vinara Yanga wamefunga idadi hii ya mabao, na ndiyo timu inayoongoza kwa kupachika mabao mengi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**29 -** Namungo FC ina idadi hii ya pointi hizi ilikamata nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi mpaka sasa.

**28 -** Hizi ni pointi za Azam FC mpaka sasa, inayoshika nafasi ya nne kwenye msimamo wa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**27-** Ni mabao ya kufungwa ya Ruvu Shooting ambayo ipo kwenye nafasi ya 13 ya msimamo wa ligi.

**26 -** Hii ni idadi ya mabao ya Namungo ambayo mpaka sasa imeng'ang'ania nafasi ya tatu ya msimamo.

**25 -** Timu ya Mbeya City ina idadi hii ya pointi, ikiwa inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi

**23 -** Hii ni idadi ya mabao ya kufunga ya timu za Simba na Azam FC kila moja.

**21 -** Jumla ya timu tatu za Ligi Kuu zinamiliki idadi hii ya pointi kila moja. Timu hizo ni Ruvu Shooting iliyo kwenye nafasi ya 11, Coastal Union nafasi ya 12 na Dodoma Jiji ambayo ipo nafasi ya 13.

**20 -** Haya ni mabao ya kufunga ya KMC, ambayo mpaka sasa ipo kwenye nafasi ya tisa ya msimamo ya ligi.

**18 -** Mbeya City, Azam FC, Biashara United na Mtibwa Sugar zimeruhusu idadi hii ya mabao kwenye wavu wake kila moja.

**17-** Timu ya Mbeya Kwanza na Biashara United zimepachika idadi hii ya mabao mpaka sasa.

**12-** Ni idadi ya mechi ambazo Simba imepata ushindi msimu huu kwenye mechi 19 ilizocheza.

**11-** Ni idadi ya mechi ambazo Prisons imepoteza kwenye Ligi Kuu, ikiwa ndiyo timu iliyopoteza idadi nyingi zaidi.

**10-** Biashara United, Polisi Tanzania na Mbeya City ndizo timu zilizokuwa na sare nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Na hii ndiyo idadi ya sare ya kila timu.

## JE, WAJUA?



BAO la Lionel Messi la dakika ya 68 wakati Paris St-Germain ikilazimishwa sare ya bao 1-1 na Lens juzi kwenye mechi ya Ligue 1, limeiwezesha kufikia rekodi ya kutwaa taji la 10 la Ufaransa ikiwa imebakiza mechi nne kabla ya msimu kumalizika.





# Mahakama 10 za mfano kujengwa maeneo mbalimbali

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAHAKAMA 10 za mwanzo za mfano zinatarajiwa kujengwa kwenye maeneo mbalimbali ikiwa ni utekelezaji wa Mpango Mkakati wa awamu ya pili wa maboresho ya mahakama nchini ulioanza mwaka 2020 hadi 2025.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama nchini, Prof. Elisante Ole Gabriel alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika Kijiji cha Haubi Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma ambacho ni miongoni mwa maeneo yatakayojengewa mahakama hizo.

Alisema kati ya mahakama hizo mbili zitajengwa Dodoma katika Kijiji cha Kinusi wilaya ya Mpwapwa na Haubi.

"Hivi sasa tupo katika mpango mkakati wa awamu ya pili, katika mpango mkakati huu kutakuwa na maboresho kwani hadi sasa Tanzania kuna Mahakama za Mwanzo 960 huku mahitaji yakiwa ni 3,900 hivyo bado kuna upungufu," alisema Prof. Gabriel. Alisema Jaji Mkuu Prof. Ibrahim Juma, alielekeza kuwa ni vyema kuangalia namna ya kujenga mahakama za mwanzo kwa kuzingatia maeneo ambayo ni vigumu wananchi kupata huduma za mahakama. Mtendaji huyo alisema serikali itajenga jengo jipya la mahakama ya mwanzo na nyumba mbili za watumishi ambao wanahitaji ardhi isiyopungua ekari mbili.

Alihamasisha wananchi kujitolea kwa kushiriki shughuli za ujenzi.

Kwa upande wake, Diwani wa Kata ya Haubi, Paul Irovya, alisema mahakama iliyopo ilijengwa kabla ya Uhuru na majengo yake yamechakaa yanahitaji matengenezo au kujenga upya. Alisema ujenzi wa mahakama yenye hadhi itakuwa ni jambo jema kwa sababu itawapunguzia wananchi mzigo wa kusafiri umbali mrefu kwa ajili ya kutafuta haki.

"Tunaishukuru serikali kwa maono yake na kuamua kujenga mahakama hapa Haubi, tunaamini itakuwa na tija kwa wananchi wetu kwa sababu itawarahisishia na kuwapunguzia mzigo mkubwa waliokuwa wamebeba wa kusafiri umbali mrefu," alisema Diwani.

Naye, Mwenyekiti wa Kijiji cha Haubi, Anasi Lubuva, alisema licha ya kuwapo kwa mahakama hiyo iliyochakaa, hakuna hakimu kutokana na aliyepo kuhudumia mahakama zaidi ya mbili.

Pia, alisema kero nyingine ni Mabaraza ya Kata yaliyopo hayana ujuzi wa namna ya kuendesha kesi, wakati mwingine wanaendesha kwa uzoefu sio kwa kufuata sheria na kushauri kuandaliwa semina maalumu kwa ajili ya kufundishwa namna ya kuendesha kesi.

"Tuna changamoto ya kukosa hakimu na aliyepo anahudumia mahakama zaidi ya mbili hivyo kuna wakati wananchi wanakuwa wana muhitaji, lakini kutokana na majukumu anashindwa kufika," alisema.



Katibu wa Oganaizesheni Jumuiya ya Wazazi Taifa Chama Cha Mapinduzi, Said Kingengene akizungumza na wajumbe wa jumuiya hiyo wa wilaya ya Chemba (hawapo pichani) jana wakati wa ziara yake kuangalia mwenendo wa uchaguzi ngazi ya matawi na kata. Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi ya CCM (katikati) wilaya ya Chambe Hamadi Haji, (kushoto) Katibu wa Wazazi CCM Mkoa wa Dodoma Watende Amri. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Viongozi CCM watakiwa kuhamasisha wanachama kugombea nafasi matawi

**Na Peter Mkwavila,** KONDOA

VIONGOZI wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wilayani Kondoa, wametakiwa kuhamasisha wanachama wao kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi unaofanyika kwenye ngazi za matawi na kata.

Mkuu wa Idara ya Oganaizesheni wa Jumuiya ya Wazazi wa chama hicho Taifa, Said King'eng'ena, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na viongozi wa CCM kwenye ziara ya kuangalia mwenendo wa uchaguzi wilayani humo.

Aliwataka viongozi hao kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wanachama wao ili kujitokeza kwa wingi kugombea kwenye uchaguzi huo ambao umeshaanza ngazi ya mashina.

Alisema kuwa badala ya tabia iliyojengeka kwa baadhi ya viongozi ya kuwaweka wanachama wao kwa maslahi yao, watumie muda huo kuwahamasisha wajitokeze na kugombea nafasi hizo.

"Hapa nataka niseme kuwa kuna baadhi ya viongozi ndani ya chama, wamekuwa na tabia ya kuweka safu yao ya viongozi wanaowataka hata kama hawana uwezo, tabia hii inakigharimu chama chetu kwa kuwa viongozi wanaowekwa hawana sifa," alisema.

Naye, Katibu wa Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Dodoma, Watende Amri, alisema chama kwa kufanya mabadiliko madogo ya marekebisho ya Katiba ambayo hivi sasa imeipa fursa kwa viongozi wa jumuiya kushiriki kwenye mikutano mikuu ya CCM ngazi ya tawi, kata na wilayani.

Alisema kuwa hivi sasa CCM ipo kwenye uchaguzi wa ngazi ya matawi na kata kwa ajili ya kuwapata viongozi wake.

Alitaja viongozi hao wanaochaguliwa kwenye matawi na kata ni Wenyeviti, Makatibu, Wajumbe wa kamati ya utekelezaji, makatibu wa elimu malezi na mazingira, mjumbe wa mkutano mkuu wa wilaya ya Halmashauri Kuu pamoja na wawakilishi wa Idara ya Wanawake na Vijana.

# Makinda ataka CCWT kuhamasisha ushiriki sensa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Sensa Taifa, Spika mstaafu wa Bunge, Anne Makinda, amekitaka Chama cha Wafugaji nchini (CCWT), kuhamasisha wafugaji kushiriki kwenye sensa inayotarajiwa kufanyika Mwezi Agosti mwaka huu ili serikali itambue ukubwa wa sekta hiyo.

Makinda alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki katika mkutano maalum wa chama hicho uliofanyika jijini hapa.

Alisema ili serikali itatue kero za sekta ya ufugaji ni lazima ifahamu idadi ya wafugaji, ukubwa wa kaya za wafugaji ikiwamo sehemu wanayopatikana.

"Naomba msiachie serikali peke yake katika zoezi la kuhamasisha sensa bali wote tunapaswa kutoa mchango wetu katika kuhamasisha sensa ya watu na makazi," alisema Makinda.

Aliwataka viongozi wa CCWT kuhakikisha wanawasisitiza wafugaji kutoa ushirikiano wa kujibu maswali pindi muda wa sensa utakapowadia.

"Tunataka sensa hiyo serikali ipate takwimu muhimu ambazo zitatumika kufanya maamuzi sahihi ya namna ya rasilimali za nchi zitakavyotumika," alisema.

Makinda alisema kuna jamii nyingine hazipendi kuulizwa maswali kama vile kutaja idadi ya mifugo, idadi ya watoto, hivyo viongozi wa wafugaji waliochaguliwa kutoka kila kanda wafanye jitihada ya kuwaelimisha itakapofika siku ya kuhesabiwa.

Naye, Mwenyekiti wa CCWT, Jeremiah Wambura, alisema watahakikisha elimu ya umuhimu wa Sensa inafikia jamii ya wafugaji ili washiriki kikamilifu kuhesabiwa.

Alisema kufanya hivyo, kutaisaidia sekta ya ufugaji kujulikana idadi yao jambo ambalo litaisaidia serikali kufanya maboresho ya sera ambazo zitasaidia kutatua kero zilizopo ndani ya sekta hiyo.

"Tuna kila sababu ya kutoa ushirikiano Mwenyekiti na Spika mstaafu usiwe na wasiwasi juu ya ushiriki wa wafugaji katika Sensa ya Watu na Makazi iliyopangwa kufanyika Agosti 23, mwaka huu," alisema.



# OSHA yahimiza usalama kwenye migodi

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

WAKALA wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, imewataka wamiliki wa migodi ya kuchimba dhahabu kuhakikisha wanawanunulia vifaa vya kujikinga na majanga wafanyakazi wao, pindi wanapokuwa kwenye shughuli za uchimbaji ili kuwakinga na athari za kiafya pamoja na usalama wao.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Mkaguzi wa Afya na Mazingira kutoka OSHA, Renatus Qalqal, wakati akikagua shughuli za uchimbaji madini ya dhahabu katika mlima Elizabeth ulioko eneo la Saza Mkwajuni wilayani Songwe.

Alisema baada ya kukagua na kujionea shughuli za uchimbaji ameona wafanyakazi wengi ambao amedai ni vibarua kutokupewa vifaa vya kutosha ili kujikinga na athari wanapokuwa kwenye uchimbaji wa madini ya dhahabu.

“Wafanyakazi wengi wa migodi ya dhahabu hawana vifaa vya kutosha wanapokuwa kwenye shughuli zao, jambo ambalo linahatarisha afya za watu, nawaomba wamiliki wa migodi kuwajali wafanyakazi kwa sababu ni haki kupewa vifaa vyote wanapokuwa kwenye shughuli za uchimbaji madini,” alisema Qalqal.

Aidha alisema mmiliki yeyote ambaye baada ya maagizo hayo hatanunua vifaa vya kutosha kwa wafanyakazi wake atakuwa anatafuta adhabu kwa mujibu wa sheria za Osha.

Alisema kila mmiliki wa mgodi anapewa maelekezo ya namna ya kufanya ili kuhakikisha usalama na afya kwa wachimbaji kwa wafanyakazi, mmiliki na jamii inayowazunguka na kwamba Osha hufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo hayo ili kuangalia utekelezaji wa sheria hizo.

Baadhi ya wachimbaji wa madini ya dhahabu katika mlima Elizabeth walisema wanafanya kazi katika mazingira magumu kwani hakuna vifaa vinavyowawezesha kutimiza majukumu yao kwa usalama na amani.

Walisema wamiliki wa migodi eneo hilo hawajali usalama wao badala yake wanahitaji wafanyakazi watafute dhahabu bila kujali afya zazo.

Aliiomba Osha kukaa na wamiliki wa migodi waambiwe mambo wanayopaswa kuwafanyia wafanyakazi wao ikiwamo ununuzi wa vifaa vya kisasa pamoja na ujira mzuri ili nao waweze kutunza familia zao ambazo walidai wameziacha nyumbani.

Mratibu wa mafunzo kutoka Osha, Charles Niima, aliwataka wamiliki wa migodi na wafanyakazi kuzingatia usafi na usalama kwenye maeneo yao ya uchimbaji madini ili kujikinga na magonjwa ya milipuko kama kipindupind na homa ya matumbo.




Fundi mitambo ya kukamata madini ya dhahabu, Hassan Hance, kutoka kampuni ya uchenjuaji madini hayo Daniel Elution akihakiki mitambo tayari kwa ajili ya kuendelea na shughuli hizo juzi. **PICHA NA GRACE MWAKALINGA**

# Maelfu Mbarali kupata huduma za uhakika afya

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

ZAIDI ya wakazi 40,000 wa kata za Mahongole, Mwatenga, Kongolo na Igurusi wanatarajia kupata huduma za matibabu kama huduma za wajawazito, upasuaji, tiba kwa wenye maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) baada ya kukamilika kwa Kituo cha Afya cha Mahongole.

Kwa mujibu wa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Dk. Godfrey Mwakalila, hadi sasa ujenzi wa kituo hicho umefikia asilimia 90.

Alisema Serikali imetoa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo hicho na kwamba fedha hizo wamezipokea kwa awamu mbili, awamu ya kwanza walipokea Sh. milioni 250 ili kujenga jengo la wagonjwa wa nje (OPD), maabara na kichomea taka.

Alisema ujenzi wa majengo ya awali ya OPD, maabara na kichomea taka ulianza Novemba Mosi mwaka 2021 na unatarajiwa kukamilika Aprili 30 mwaka huu.

“Tunaishukuru serikali yetu kwa kutupatia fedha milioni 500 kujenga kituo kikubwa cha afya hapa kata ya Mahongole, wananchi zaidi ya 40,000 watanuifaka na huduma za matibabu hapa kwa sababu fedha tulizopatiwa zinatokana na tozo za miamala ya simu,”alisema Dk. Mwakalila.

Aliongeza kuwa hadi sasa wametumia Sh. milioni 128 kati ya milioni 500 zilizotolewa na serikali na kwamba wananchi wamechangia nguvu zao kama mchanga, tofali, mawe, kujaza kifusi kwenye msingi na usafi eneo la ujenzi jumla ikiwa ni Sh. milioni tisa.

Alisema wameanza kujenga majengo ya awamu ya pili ambalo ni la upasuaji, wodi ya wazazi, jengo la kufulia nguo na njia za kupitisha wagonjwa ambapo ujenzi wa majengo hayo unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni 30, mwaka huu.

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi kituo hicho, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alieleza kuridhishwa na kasi ya ujenzi na kuwahimiza mafundi kukamilisha kazi kwa wakati ili wananchi waanze kupata huduma za matibabu.

Alisema ujenzi unaridhisha na kwamba matamanio yake ni kuona wananchi wa kata zilizo jirani na kituo hicho wanapata huduma za matibabu ili kuokoa gharama za muda na fedha kwenda Hospitali ya Chimala na Hospitali ya Wilaya.

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo ili kuwasaidia wananchi kupata huduma karibu na maeneo yao.

Alisema kukamilika kwa kituo hicho kuwaokoa kina mama waliokuwa wanatumia umbali mrefu kufuata huduma za matibabu maeneo mengine.

“Rais wetu Samia Suluhu Hassan ametutua mzigo mkubwa tulikuwa nao viongozi na wananchi katika kuchangia shughuli za kijamii ikiwamo ujenzi wa vyumba vya madarasa, maeneo ya kutolea huduma za matibabu, miundombinu ya barabara na maji hakika tunajivunia nawaomba wananchi wa Mbarali tuunge mkono jitihada hizo kwa kutunza miundombinu hii,” alisema Mfune.

## Sababu Rungwe kuvuka lengo anwani za makazi

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Rungwe imefikia asilimia 103 na jumla ya anuani 63,926 zimekusanywa kwenye zoezi la usajili wa anuani za makazi na postikadi.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, alisema zoezi hilo limefanikiwa kwa sababu viongozi wote kuanzia ngazi ya kitongoji walipewa elimu na maelekezo juu ya umuhimu wa zoezi hilo kwa ajili ya maendeleo ya wananchi.

Alisema baada ya viongozi hao kujengewa uwezo walifanya mikutano ya hadhara kwa wananchi na kueleza faida ya zoezi hilo na hatimae kupata ushirikiano mkubwa wakati wa kutekeleza majukumu yao.

Alisema awali wakati wa zoezi hilo walikisia kufikia jumla ya anuani 63,165, lakini kutokana na hamasa kwa wananchi waliweza kufikia 63926 na kuvuka asilimia 100.

“Nawashukuru sana wananchi wangu wa Rungwe hakika mmeniheshimisha mwitikio umekuwa mkubwa na kufikia hatua hii ya zoezi la anuani za makazi, kila mmoja kwa nafasi yake ametimiza wajibu wake, lakini nawaomba bado zoezi linaendelea na kauli ya mama yetu Rais Samia Suluhu Hassan anasema zoezi hili likamilike Mei, sasa sisi Rungwe tusifikie tarehe aliyotuagiza mama tukamilishe Aprili hii,” alisema Dk. Anney.

Aliwaomba viongozi kuanzia ngazi ya kitongoji kuendelea kuhamasisha wananchi kushiriki katika zoezi hilo hasa kwa maeneo ambayo bado hayajakamilisha kwa kuhakikisha wanatoa ushirikiano wakati wa kutekeleza suala hilo.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Ilima, Amanyisye Mbukwa, alisema licha ya eneo hilo kupakana na Wilaya ya Kyela, lakini wameendelea kuhamasisha kutengeneza vibao vya anuani ya makazi ili kuifanya wilayani yao inakuwa kinara katika kutekeleza zoezi hilo.





Ofisa Mfuatiliaji wa wagonjwa wa Malaria, Faki Mlekwa Faki akitoa damu kupima mgonjwa wa Malaria, Mwanaidi Rashidi katika kijiji cha Ghana Wilaya ya Kati Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Changamoto kutokomeza malaria Zanzibar zatajwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

LICHA ya serikali ya Zanzibar kutokomeza kwa kiasi kikubwa ugonjwa wa malaria, inaelezwa kuwa bado upo kwa sababu kuna changamoto zinazozuia kumaliza kabisa ikiwamo maambukizi kwa wasafiri.

Hayo yalielezwa na Meneja Mradi wa kumaliza malaria kutoka Kitengo cha Malaria Zanzibar Muhammed Ali Abdallah wakati akizungumza na waandishi wa habari Ofisini kwake Mwanakwerekwe katika ziara iliyoratibiwa na shirika la msaada wa Marekani USAID na Kituo cha Kudhibiti na Kujikinga na Magonjwa (CDC) kwa kushirikiana na kitengo cha Malaria Zanzibar (ZAMEP).

Meneja huyo alisema taarifa za ufuatiliaji zinaonesha kuwa Wilaya za Magharibi 'A'na 'B, na Wilaya za Kati Unguja ndiyo zinazoongoza kwa wagonjwa wa malaria Zanzibar. "Hii inamaanisha kuwa maambukizi ya ugonjwa huu bado yanaendelea ndani ya Wilaya hizi. Kwa mnasaba huo wizara imo katika matayarisho ya kuendesha upigaji dawa shehia zote za wilaya hizo kwa uratibu utakaotolewa na wataalamu"anasema.

Anasema wizara ya Afya kupitia kitengo cha malaria bado inaendelea kusisitiza kutumia mikakati ya kupambana na malaria ambayo imeonesha mafanikio makubwa.

Alitaja mikakati hiyo ni matumizi ya vyandarua vilivyotiwa dawa, tiba sahihi ya malaria kwa kutumia dawa mchanganyiko, upigaji dawa majumbani , ufuatiliaji wagonjwa majumbani kwa lengo la kuwabaini walio na maambukizi, usafi wa mazingira kwa lengo la kuondosha mazalio ya mbu na kuwatumia wahudumu wa afya ya jamii katika ngazi ya shehia (CHV).

Naye Ofisa Uchunguzi wa Vimelea vya Malaria, Safia Muhammed, anasema kuna vifaa vya upimaji wa malaria katika Bandari ya Malindi Unguja na viwanja vya ndege ili wasafiri kupima vimelea hivyo kudhibiti maambukizi mapya.

"Suala la kupima malaria kwa wasafiri ni hiyari hivyo wasafiri huhamasishwa wapime na kwa mwaka 2011 wasafiri 11 waligundulika kuwa na malaria baada ya kupimwa,"alisema.

Alisema Malaria imehama kwa watoto wadogo walio chini ya umri wa miaka mitano kwa sababu bado hifadhi ya kujikinga malaria ikiwemo kutumia vyandarua ipo zaidi kwa watoto wa rika hizo.

Alisema wanatarajia sheria ya afya ya jamii, kufanyiwa marekebisho ili kutumika katika kutoa elimu kuhusu utoaji wa huduma katika kujikinga na malaria.

Juma Hassan Mcha, Mdhibiti wa Mbu katika Kitengo cha kudhibiti malaria, alisema baada ya kuwapo kwa malalamiko kuhusu dawa ya kuulia mbu majumbani iliyokuwa ikitumika kuwa na athari kwa jamii ikiwamo muwasho wakaibadilisha.

"Hivi sasa tunatumia dawa mpya ambayo inaitwa Sumishield haina madhara wala athari yoyote na tumeacha kutumia dawa ya Labda cylothreen ambayo ilikuwa ikilalamikiwa sana, "alisema.

Naye Daktari wa Kituo cha Afya Kianga, Wilaya ya Magharibi A Unguja, Dk Salma Muhammed Hemed, alisema kuwa wagonjwa 1500 waliopimwa malaria kwa mwaka 2021, 23 waligundulika kuwa na malaria na kati ya hao 20 walikuwa ni wasafiri ambao walitoka Unguja kwenda Tanzania Bara na kurudi Zanzibar.

Alisema kituoni hapo wanakinga na tiba ya malaria ikiwamo matumizi ya dawa kwa mgonjwa wa malaria na utoaji wa vyandarua kwa watoto na mama wajawazito ili kujikinga na ugonjwa huo.

Daktari wa Hospitali ya Kivunge Wilaya ya Kaskazini A, Unguja, Juma Ali Makame, alisema kuwa elimu wanayoitoa kituoni hapo kuhusu malaria imesadia kupungua kwa wagonjwa kituoni hapo.

Aliongeza kuwa kati ya wagonjwa 546 waliopimwa malaria kwa Januari mwaka huu 19 walikutwa na malaria na kupatiwa matibabu wakati Febuari wagonjwa 330 waliopimwa 12 walikutwa na malaria na Machi wagonjwa tisa walikutwa na malaria kati ya wagonjwa 317 waliopimwa.

"Tukilinganisha na tulipotoka hii idadi ya wagonjwa wa malaria ni ndogo sana kwa hospitali yetu hii ya Wilaya kwa sababu elimu ya afya ya kujikinga na malaria imesaidia sana kupunguza idadi ya wagonjwa hao,"alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Kituo cha Afya Kidimni Wilaya ya kati Unguja, Rajab Haji Rajab, alisema kuwa kituoni hapo wanaibua kesi nyingi za malaria ambapo kwa mwezi huu wa Aprili wameshaibua kesi tatu za wagonjwa wa malaria na wote ni wasafiri.

Siku ya Malaria Duniani huadhimishwa kila ifikapo Aprili 25 ya kila mwaka ambapo ujumbe wa mwaka huu ni "Ewe Msafiri Chukua tahadhari Zanzibar ibaki bila ya malaria, zero malaria inaanza na mimi". lengo ni kufikia zero malaria ifikapo mwaka 2023.

# Diaspora waipiga jeki Wizara ya Afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya imepokea msaada wa mashuka na magodoro wenye thamani ya zaidi Sh. milioni 13 kutoka Umoja wa Wazanzibari wanaoishi katika Falme za Kiarabu (UAE) wenye lengo la kuleta maendeleo katika sekta ya Afya.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo huko ofisini kwake Mnazi Mmoja, Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema msaada huo utasaidia kuboresha na kuimarisha utoaji wa huduma za afya nchini

Aliushukuru umoja huo kwa kuonyesha uzalendo wa kuipenda nchi yao na kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Wizara ya Afya katika kutoa huduma bora kwa wananchi.

Aidha Waziri Mazrui, aliahidi kuusimamia vyema msaada huo na kuhakikisha kwamba unatumika ipasavyo, pomoja na kuutunza ili kutumika na kudumu kwa muda mrefu. "Niwahakikishie kuwa nitausimamia mzigo huu ili uwafikie walengwa wanaostahiki kutumia magodoro na mashuka hayo pamoja na kuyatunza ili kuishi kwa muda mrefu,"alieleza waziri huyo.

Naye Mwakilishi wa umoja huo, Mohamed Khamis , alisema kuwa wataendelea kuisaidia sekta ya afya pamoja kuwaomba Wazanzibari wengine kujitokeza kusaidia ili kuhakikisha kwamba utoaji wa huduma unaimarika nchini.

## Watendaji serikalini watakiwa kujitathmini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, amewataka watendaji wa ofisi hiyo kujitathmini na kujipanga upya katika utekelezaji wa majukumu yao ya kazi.

Amesema kwa kufanya hivyo lengo la serikali la utoaji wa huduma bora kwa wananchi litafikiwa kwa wakati.

Aliyasema hayo Kisiwani Pemba wakati akizungumza na watendaji wa Idara, Tume na Mamlaka zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika mkutano wa kujitambulisha kufuatia uteuzi wake hivi karibuni ili kuona maendeleo ya taasisi hizo.

Alisema ni wajibu wa watendaji na wafanyakazi kufanya kazi kwa bidii na kufuata mwongozo wa utumishi pamoja na kujitathmini kiutendaji, kuona kipi ambacho amekifanikisha kwa muda wa wiki nzima ambacho kimeleta tija kwa taasisi na wananchi.

Waziri Harusi aliwataka watendaji hao kuzidisha ari na nguvu ya kiutendaji kwa wananchi wanaohitaji huduma na kutatua changamoto zao ukizingatia kuwa sekta za ofisi hiyo ni mtambuka hivyo hawapaswi kukaa ofisini bali wajitoe kufikisha elimu na huduma stahiki kwa wanajamii.

"Watendaji hakikisheni mnashirikiana pamoja ili wale mnaowaongoza nao waone kuwa viongozi wao wapo makini na hakutakuwa na mwanya wa kufanya maovu, kama zipo changamoto zigeuke kuwa fursa kwa kuwa wabunifu wa mipango mipya yenye kuleta tija,"alisisitiza Harusi

Ofisa Mdhamini wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Ahmeid Abubakar, alimuahidi waziri huyo kuwa watashirikiana na watendaji na kutekeleza majukumu yao vyema, kusimamia miradi ya maendeleo na kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Waziri huyo alizitembelea Idara na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Baraza la Watu wenye Ulemavu na Tume ya UKIMWI pamoja na kukagua miradi ya maendeleo ukiwemo mradi wa ujenzi wa tuta la kuzuwia maji ya chumvi yasiingie katika mashamba uliopo Tovuni.

Pia alitembelea mradi wa ujenzi wa Ukuta wa mawe katika fukwe ya mwambao wa eneo la Msuka, mradi wa ujenzi wa mabwawa ya maji machafu ulipo Kichungwani, pamoja na kufika Likoni Kojani kuangalia eneo linalotarajiwa kujengwa ukuta wa kuzuwia mmomonyoko wa fukwe ambao pia utaunusuru mbuyu wa asili uliopo eneo hilo ambao upo hatarini kuanguka.

# Naibu Spika apongeza uwekezaji BancABC

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Spika, Mussa Azzan Zungu, ameipongeza BancABC Tanzania, ambayo ni kampuni tanzu ya Atlas Mara, kwa uwekezaji mkubwa ulioleta suluhisho la kifedha kwa Watanzania.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa futari iliyoandaliwa na benki hiyo kwa wateja wake, alisema serikali inafanya mageuzi mbalimbali tangu miaka ya 90 kwa lengo la kuiwezesha sekta binafsi kukua na kuleta matokeo chanya.

"Bunge ni washauri wakuu wa serikali tutaendelea kuhakikisha kuwa uhusiano wa karibu uliopo kati ya serikali na sekta binafsi zikiwemo taasisi za fedha unadumishwa."

Alisema tangu kuingia kwa mfumo wa soko huria nchini, sekta binafsi ilichukua nafasi yake katika huduma mbalimbali zikiwamo huduma za sekta ya kifedha.

"Sekta ya fedha ni nyenzo muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa taifa lolote lile, hivyo unapokuwa na sekta imara ya fedha maana yake ni kwamba uchumi wa nchi unakuwa imara. Serikali inatambua jitihada za kukuza uchumi na kupunguza umaskini kuwa na mafanikio bila kushirikisha sekta binafsi hususan taasisi za kifedha," alisema.

"Natambua kuwa BancABC imeendelea kuwa mdau mzuri sana kwenye kuunga mkono juhudi na mikakati ya serikali ya kuongeza tija katika sekta ya huduma za kifedha kwa kupanua huduma zenu ili kuwafikia Watanzania walio wengi zaidi," alisema.

"Naomba niwapongeze sana BancABC kwa juhudi zenu kubwa mnazo weka kwenye kupanua huduma zenu ili kuwafikia Watanzania walio wengi na hasa kwenye maeneo ya vijijini. Hii ni hatua kubwa na ya kupongezwa kwani kadri mnavyoendelea kuwafikia Watanzania wengi ndipo mnapozidi kuwafungulia milango ya kujiongeza kiuchumi na hivyo kuunga mkono juhudi za serikali za kuongeza kipato kwa wananchi wake," Naibu Spika Zungu alisema.

Alisema anatambua benki hiyo inashiriki utekelezaji wa masuala ya kijamii ikiwemo kutoa huduma ya bima ya afya kwa watoto yatima, kushirikiana na Taasisi ya Stella Ikupa, kukuza uelewa wa huduma jumuishi za kifedha kwa watu wenye ulemavu pamoja na kushirikiana na TAMISEMI katika ujenzi wa vyoo na vyumba vya madarasa ya shule mbalimbali nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa BancABC Tanzania, Imani John, alisema kuwa BancABC inatoa huduma mbalimbali kwa watu binafsi, wajasiriamali wadogo na wa kati pamoja na wateja wakubwa zikiwamo huduma za kuweka fedha pamoja na mikopo wezeshi kwa wateja wa madaraja yote.

Kwa kipindi ambacho tumekuwa tukitoa huduma, ubunifu wa huduma za BancABC pamoja na mipango yetu madhubuti imesababisha kutambuliwa na wadau mbalimbali, kwenye sekta ya huduma za kifedha na kutoa tuzo mbalimbali.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Azzan Zungu akiwaongoza wateja na wafanyakazi wa Benki ya BancABC Tanzania kwenye futari iliyoandaliwa na benki hiyo ikiwa ni ishara ya kuonyesha upendo na shukrani hasa kwa wale ambao wako kwenye mfungo kwa kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mamia wajitokeza kupima afya kambi ya TCB Mbagala

**Na Mwandishi Wetu**

MAMIA ya wananchi jana walijitokeza kupima afya zao bure,kwenye utaratibu ulioandaliwa na Tanzania Commercial Bank (TCB) tawi la Mbagala, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kwa kushirikiana na Shirika la Bima la Alliance Insurance Corporation, ili kujali wateja wao na wananchi kwa ujumla.

Akizungumza katika hafla hiyo, Meneja wa TCB, tawi la Mbagala, Edward Mwoleka, alisema lengo ni kuhakikisha kila mwananchi anaangalia afya yake na kupata ushauri utakaomsaidia.

"Katika kuunga mkono jitihada za serikali, Tanzania Commercial Bank, imekuja na kambi maalum ya watu kupima afya na kupewa ushauri wa bure katika eneo la Mbagala," alisema na kuongeza:

"Benki ya Biashara ya Tanzania tuna kila sababu ya kuwajali Watanzania na kuwapa wanachotamani ndiyo maana leo tumeungana na wenzetu wa Alliance Insurance Corporation kwa kutoa huduma ya kufanya vipimo vya magonjwa mbalimbali bure."

Aidha, Mwoleka aliwataka Watanzania kujiunga na benki hiyo kwa kuwa inatoa huduma zinazotatua changamoto za Watanzania wengi.

"Tuna mikopo ya kuanzia mfanyabiashara mdogo, wa kati na mkubwa, pia tunatoa kwa wastaafu niwasihi wateja wetu wajitokeze kuja kupata huduma katika benki yetu pendwa," alisema.

Kwa upande wake Msemaji wa Alliance Insurance, Justin Erick aliishukuru TCB kwa kuwaamini na kufanya kazi pamoja ili kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa wananchi.

**Tuna mikopo ya kuanzia mfanyabiashara mdogo, wa kati na mkubwa, pia tunatoa kwa wastaafu niwasihi wateja wetu wajitokeze kuja kupata huduma katika benki yetu pendwa.**

## TAMWA yakumbusha waandishi kuheshimu taaluma yao

**Na Said Hamdani,** MTWARA

CHAMA cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kimewataka waandishi wa habari kujenga tabia ya kuheshimu taaluma na vyombo wanavyovitumikia kwa kuvaa mavazi ya staha wanapotekeleza majukumu yao.

Rai hiyo imetolewa na Saumu Bakari wakati wa semina ya kuwajengea uwezo na kuutambulisha mradi mpya wa TAMWA kwa waandishi wa habari, mikoa ya Mtwara na Lindi, iliyofanyika Manispaa ya Mtwara-Mikindani.

Mradi huo unajulikana kama 'Woman in Media' ni wa miaka mitano ulioanza mwaka 2021 hadi 2024 na unafadhiliwa na wadau wa maendeleo (VIKES) wa nchini Finland.

Bakari akiwasilisha mada katika semina hiyo, alisema kumekuwa na tabia kwa baadhi ya waandishi, wakiwamo wanawake kutoitendea haki taaluma yao, ikiwamo mavazi, hali inayodhalilisha taaswira ya taaluma ya habari.

Alisema uandishi wa habari ni taaluma inayotegemewa na watu wa rika mbalimbali ndani na nje ya mipaka ya Tanzania na kwamba kutoitendea haki ni kosa linaloweza kusababisha jamii kuwadharau na vyombo wanavyovitumikia kuviona vya ovyo.

"Ndugu zangu taaluma ni kubwa na inategemewa na kila mmoja wetu, wazee, vijana hivyo tuitendee haki," alisistiza Swaumu.

Alisema ni vyema waandishi wakajitafakari kwa kuwa nadhifu katika mavazi ili kulinda na kujenga heshima kama wanataaluma na vyombo wanavyovitumikia.

Kauli hiyo iliungwa mkono na Katibu Msaidizi wa Klabu ya waandishi Mkoa wa Mtwara, Gregory Milanzi, kuwa inashangaza kuona mwandishi akitoka nyumbani na kwenda ofisini amevaa suruali fupi au ndefu chini ya makalio huku miguuni amevalia viatu vya yebo yebo.

"Umeshafika ofisini na Mhariri anakutuma uende Ikulu, utaenda ukiwa kwenye hali hiyo kweli?" Alihoji Milanzi.

Mafunzo hayo ya siku moja yaliyoendeshwa na TAMWA yalishirikisha zaidi ya waandishi 25 kutoka mikoa ya Lindi na Mtwara, yaliyokuwa na lengo la kuwaongezea uwezo na kuutambulisha Mradi mpya unaoangalia usawa wa jinsia kwa wanahaabri unaofadhiliwa na wadau wa maendeleo (VIKES) ya nchini Finland.

HABARI KIMATAIFA

## Mlipuko waua 80 Nigeria

**Lagos,** NIGERIA

WATU 80 wameteketea kwa moto kutokana na mlipuko uliotokea usiku katika kiwanda kinachochakata mafuta kinyume cha sheria kusini mwa Nigeria.

Taarifa hii ni kwa mujibu wa Kitengo cha kukabiliana na Matukio ya Dharura.

Mwakilishi wa Kitengo cha Taifa cha Kukabiliana na Majanga (NEMA), Ifeanyi Mnaji, aliliambia shirika la habari la Ufaransa AFP kwamba miili ya watu hao 80 imekutwa imeteketea kwa moto katika eneo la tukio.

Alisema pia katika eneo hilo kumeshuhudiwa kutapakaa kwa magari yaliyoungua vifaa vya kuchotea mafuta, vilivyotumika kuibia mafuta ghafi na petroli.

Vyombo vya habari nchini Nigeria vimesema zaidi ya watu 100 wamekufa kutoka na mlipuko huo.

Usafishaji haramu wa mafuta ni jambo la kawaida katika ukanda huo wa mafuta ambako wezi huharibu mabomba ili kuiba mafuta ghafi ambayo wanayasafisha ili kuyauza kwenye soko la magendo. **DW**

## Macron, Marine Le Pen wachuana urais

**Paris,** UFARANSA

WAFARANSA wamepiga kura kumchagua rais wa kuliongoza taifa hilo. Uchaguzi huu wa marudio unafanyika kwa sababu katika duru ya kwanza wiki mbili zilizopita, hakuna aliyepata zaidi ya asilimia 50 ya kura.

Rais Emmanuel Macron (pichani) anatafuta muhula wa pili, anapewa nafasi kubwa ya kuibuka mshindi, baada ya wadadisi wa siasa kusema vema kwenye mjadala wa televisheni wiki hii dhidi ya Le Pen.



Hata hivyo, uchaguzi huo pia unaelezwa kuwa na ushindani mkali kinyume na ilivyokuwa mwaka 2017, huku Marine Le Pen akisema ana imani ya kuibuka mshindi licha ya sera zake, ambazo zinaonekana kuwa si rafiki hasa barani Ulaya.

Vituo vya kupigia kura, vilifunguliwa kuanzia saa mbili asubuhi saa za Paris na kufungwa baada ya saa 12 na matokeo yatafahamika baadaye.



Mwai Kibaki akiwa ofisini enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

# Aprili 29 Wakenya kushiriki mazishi kitaifa Mwai Kibaki

**Nairobi,** KENYA

KENYA imetangaza siku ya Ijumaa, Aprili 29, mwaka huu kuwa ni ya mapumziko, kutoa nafasi ya kufanyika kwa ibada ya mazishi kumsindikiza Rais mstaafu Mwai Kibaki.

Waziri wa Usalama, Fred Matiang'i ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Kuandaa Mazishi, alisema kwamba siku hiyo imetengwa mahsusi kwa Wakenya kutoa heshima zao za mwisho kwa Kibaki.

**Ibada ya kitaifa ya wafu itafanyika katika Uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Nyayo jijini Nairobi.**

Rais huyo wa tatu wa Jamhuri ya Kenya atazikwa nyumbani kwake eneo la Othaya, Nyeri , Jumamosi wiki hii.

Ibada ya kitaifa ya wafu itafanyika katika Uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Nyayo jijini Nairobi.

Mwili wa mwendazake umehifadhiwa katika hifadhi ya maiti ya Lee, Nairobi.

Kibaki, alifariki Ijumaa asubuhi, Aprili 22, mwaka huu katika hospitali ya Nairobi, ambako alikimbizwa baada ya kuzidiwa na ugonjwa.

"Serikali inatangaza Ijumaa, Aprili 29, 2022 kuwa Siku ya Mapumziko ili kumpa Rais Mwai Kibaki mazishi ya kiserikali," Dk. Matiang'i alisema kupitia tangazo rasmi katika toleo la kipekee la Gazeti Rasmi la Serikali.

Dk. Matiang'i alisema kuwa hafla ya mazishi ya Kibaki itaendeshwa kwa taadhima na kanuni za kijeshi.

# Ujumbe wa Marekani wazuru Kyiv

**Kyiv,** UKRAINE

RAIS wa Ukraine Volodymyr Zelensky, wakati akisema anakutana katika mji mkuu wa nchi hiyo na Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken, na Waziri wa Ulinzi, Lloyd Austin, Ikulu ya White House ilikataa kuzungumzia ziara hiyo.

Maofisa wa Ukraine walisema vikosi vya Russia vilijaribu kuvamia kiwanda cha chuma kinachowahifadhi wanajeshi na raia mjini Mariupol katika jaribio la kusambaratisha upinzani wa mwisho mjini humo.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari, Zelensky alitoa maelezo kidogo kuhusu maandalizi ya mkutano huo lakini alisema alitarajia matokeo madhubuti, sio zawadi tu au aina fulani ya keki, tunatarajia vitu maalum na silaha mahsusi."

Itakuwa ni safari ya kwanza ya maofisa wa ngazi ya juu wa Marekani kwenda Kyiv tangu vita vilipoanza Februari 24, mwaka huu.

Akiwa ziarani Poland mwezi Machi, Blinken aliingia kwa muda mfupi katika ardhi ya Ukraine kukutana na waziri wa mambo ya nje wa nchi hiyo.

Mkutano wa mwisho wa Zelensky wa ana kwa ana na kiongozi wa Marekani ulikuwa Februari 19 mwaka huu na Makamu wa Rais Kamala Harris.

Mpatanishi Mwandamizi kwa upande wa Ukraine na Mshauri wa Rais, Mykhailo Podolyak, jana alisema majeshi ya Russia, bado yanaendelea kuushambulia mji wa Mariupol na kuhimiza Russia kutekeleza makubaliano ya kuweka chini mtutu wa bunduki katika kipindi cha Pasaka ya madhehebu ya Orthodox

Kupitia ukurasa wake wa Twitter Podolyak alisema Russia, inaendelea kuishambulia Mariupol Azovstal. Eneo ambalo linajumuisha makazi ya raia na jeshi.

"Wanashambulia kwa makombora mazito ya anga na mizinga".

Mshauri huyo wa rais pamoja na kuhimiza utii wa makubaliano ya kusitisha mapigano katika kipindi cha Pasaka, ametaka pia Russia ifungue njia salama ya manusura na duru maalumu ya mazungumzo.

## HABARI MICHEZO

# SIMBA IKISAJILI WAPYA 10 ITATISHA AFRIKA-JULIO

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA na mchezaji wa zamani wa Klabu ya Simba, Jamhuri Kihwelo 'Julio', amesema ili timu hiyo ifanye vizuri msimu ujao kwenye michuano ya kimataifa, inahitaji kufanya usajili wa wachezaji wapya wasiopungua 10 ili kurudisha makali yake na zaidi ya pale ilipokuwa ipo juu.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, Julio ambaye kwa sasa ni Kocha Msaidizi wa Namungo FC, amesema imefika wakati kikosi hicho kinahitaji marekebisho na kuacha kuwa na wachezaji wanaocheza kwa mazoea na majina.**


Julio aliyehudumu kwenye timu hiyo kama mchezaji miaka ya mwanzoni mwa 1990 hadi katikati, baadaye kuwa Kocha Mkuu na Msaidizi kwa nyakati mbalimbali, alisema ili timu hiyo iwe na kikosi kipana, na kitakachokuwa na uhakika wa kufanya vema kimataifa ni lazima sasa kifanyiwe marekebisho baada ya misimu minne ya mafanikio na kuwa na idadi kubwa ya kikosi kile kile.

"Ukweli ni kwamba Simba kwa sasa inatakiwa kufanyiwa marekebisho, siyo twende na majina au mazoea. Nafikiri jambo hilo viongozi wanalifahamu, lakini kwa sasa hawawezi kuwaambia watu kuwa tutatoa mchezaji huyu, tutaingiza yule, nani abaki nani atoke, kwa sababu watawavunja nguvu kwani wapo kwenye mashindano. Kimsingi wanawaacha ili waendelee kupambana hadi mwisho wa msimu, na baada ya hapo wapatikene wachezaji watakuja wa kuongeza nguvu," alisema.

Alisema timu kubwa kama Simba ambayo kwa sasa imekuwa ina jina kubwa kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika, haitakiwi iwe na baadhi ya wachezaji ambao wasipokuwapo basi mashabiki wanakuwa na wasiwasi kwani hiyo siyo dhana ya kikosi kipana.

"Kwangu mimi Simba inatakiwa isajili wachezaji wasiopungua 10, nitoe mfano mimi siwezi kumtumia kipa mmoja kila siku, timu kama Simba inatakiwa iwe na makipa wanaolingana uwezo ili mmoja kama hayupo, majeruhi au kadi, basi watu wasiwe na wasiwasi, ili Manula kana kama ana matatizo basi kunakuwa hakuna shaka, lakini leo hii kila mechi kipa, huyo huyo ni woga kwa sababu makipa wengine hawawaamini, sasa hiyo huwezi kuiita timu bora au yenye kikosi kipana ambacho wao wanajinasibu. Unapokuwa na kikosi kipana, basi mchezaji yeyote anatakiwa acheze," alisema.

MCHEZAJI BORA...




Mkuu wa Kitengo cha Mahusiano ya Umma wa Benki ya NBC, Godwin Semunyu (kushoto), akikabidhi mfano wa hundi ya Sh.milioni moja kwa mchezaji bora wa mwezi Desemba, Reliant Lusajo wa Namungo FC, kabla ya kuanza kwa mchezo wao wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Yanga katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## 'Betika Mtoko wa Kibingwa' droo leo

**Na Saada Akida**

WAKATI homa ya watani wa jadi, Simba dhidi ya Yanga ikipanda moto, washindi 23 wamepatikana kwenye droo ya 'Betika Mtoko wa Kibingwa' na leo Jumatatu droo ya mwisho ya kutafuta mshindi mmoja kukamilisha idadi ya mashabiki 24 ikitarajiwa kufanyika.

Mashabiki hao 24 Jumapili wiki hii watashuhudia mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara bure itakayopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, kwa udhamini wa Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya Betika.

Akizungumza na gazeti hili jana Meneja Masoko wa Kampuni ya Betika, Nelson Mwanuzi, alisema shindano la Betika Mtoko wa Kibingwa linafika tamati leo kwa kukamilisha droo ya kupata mshindi mmoja atayeungana na wengine 23 ambao wataenda kushuhudia mechi hiyo ya Yanga dhidi ya Simba kwa kugharamiwa kila kitu.

## KMKM wakishinda 2 kutangazwa bingwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VINARA wa Ligi Kuu Zanzibar, KMKM, wameendelea kujifua wakijiandaa na michezo ya ligi hiyo itakayoendelea mapema Mei 13, mwaka huu.

KMKM wapo kileleni mwa ligi hiyo wakiwa na alama 10 zaidi dhidi ya wapinzani wao wa karibu, JKU, wanaweza kutawazwa kuwa mabingwa endapo tu watashinda michezo yao miwili kati ya mitano iliyosalia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mabaaria hao wa KMKM, Ame Msimu, alisema wanaendelea na mpangilio wao wa mazoezi katika Uwanja wa Mau ili kuhakikisha wanafanya vizuri pale ligi itakaporejea.

Alisema michezo mitano iliyobaki itakuwa migumu kuliko iliyopita kwa kuwa hiyo ndio itakayoenda kumtamlisha bingwa wa msimu huu.

# *TAMISEMI, Mambo ya Ndani zang'ara riadha*

**Na Renatha Msungu,** Dodoma

TIMU za Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na ile ya Wizara ya Mambo ya Ndani, zimeng'ara kwenye mchezo wa riadha kwa kuibuka mshindi wa kwanza na wa pili, katika michezo iliyofanyika Uwanja wa Jamhuri jijini hapa.

TAMISEMI imeshiriki mbio za mita 100, 200, 400, 800, 1,500 na 3,000, kupokezana vijiti mita 100x4, ikiwamo kurusha tufe kwa wanawake na wanaume na kujikusanyia alama 50 baada ya kupata medali za dhahabu, fedha na shaba. Wachezaji Nuru Mkomsoh amekuwa wa pili kwa wanawake na kutwaa medali ya fedha katika mbio za mita 3,000, wakati Salome Ruvanda naye katwaa fedha katika mita 100, huku Akson Mbugi na Nuru Mhomsoh wakitwaa medali za fedha katika mbio za mita 1,500 wakati Tegemea Mbogela katwaa medali ya dhahabu kwa wanawake katika mita 400.

Akson na Nuru walitwaa tena medali ya fedha katika mbio za mita 800, kabla ya Akson aliyekuwa akiongoza kutwaa tena medali ya dhahabu katika mbio za mita 200, huku Salome kwa mara nyingine akitwaa medali ya fedha katika mita 200 kwa upande wa wanawake wakati Neema Chongoro yeye alitwa medali ya dhahabu katika mchezo wa kurusha tufe huku Liuitiko Mwasere akibeba medali ya shaba katika mchezo huo.

Timu ya Wizara ya Mambo ya Ndani iliyoongozwa na wanariadha wake wa kimataifa walishika nafasi ya pili kwa kujikusanyia alama 35, ambao ni Mariam Salum na Basil John waliotwaa medali za dhahabu katika mita 3,000, 1,500 na 800, wakati Mariam safari hii akitwaa medali ya dhahabu katika mita 100 na 200 na Basil medali ya dhahabu katika mita 400.

Timu ya Uchukuzi SC wameshika nafasi ya tatu kwa kupata alama 29, ambapo wanariadha wake Shagi Luguwa walitwaa medali ya dhahabu katika mbio za mita 100 wanaume; huku Gift Kisaka akitwaa medali ya shaba katika mbio za mita 1,500; naye Aidan Adrian akitwaa medali ya fedha katika mbio za mita 400 na Anna Charles akiibuka na medali ya shaba katika mbio za mita 400.

Katika mbio za mita 200 Baraka Kinguru alitwaa medali ya shaba huku mchezo wa kupokezana vijiti kwa mita 100x4 timu ya Uchukuzi wakitwaa medali ya fedha kwa wanawake na wanaume; wakati katika mchezo wa kurusha tufe Joseph Mwambipile akitwaa medali ya fedha na daktari Hawa Senkoro mwenye umri wa miaka 58, akitwaa medali ya dhahabu kwa kuibuka wa kwanza katika mbio za mita 100 kwa watu wenye umri wa kuanzia miaka 50.

Nayo timu ya Shirika la Umeme nchini (TANESCO), imeshika nafasi ya nne kwa kujikusanyia alama tano baada ya wachezaji wake Grace Mushi kutwaa medali ya shaba katika mbio za mita 3,000, huku Grace tena akitwaa medali kama hiyo katika mita 800 na 1,500; wakati kwa upande wa wanaume Polycarp John akitwaa medali ya fedha kwenye mbio za mita 100.

Timu za Wizara ya Maji na Wizara ya Kilimo zote zimefungana pointi nne kila mmoja, huku Wizara ya Maliasili na Utalii, Shirika la Maendeleo ya Petrol nchini (TPDC), Mzinga, Wakala wa Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) zote zikiambulia alama tatu kila moja.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ERIKSEN ATAKIWA UNITED

KIUNGO wa kati wa Denmark, Christian Eriksen , 30, anatakiwa na kocha mpya wa Manchester United, Erik ten Hag. Eriksen kwa sasa yuko Brentford kwa mkataba wa miezi sita ambao utamalizika mwisho wa msimu huu. ***(Star Sunday)***

### ARSENAL KWA ABRAHAM

ARSENAL wanapania kufufu nia yao ya kumsaka mshambuliaji wa England, Tammy Abraham, 24, msimu huu wa majira ya joto na watatoa ofa ya pauni milioni 50 kwa AS Roma katika jaribio la kufikia makubaliano. ***(Star Sunday)***

### RUDIGER ANUKIA MADRID

REAL Madrid wanaongoza katika mbio ya kumsajili beki wa Ujerumani, Antonio Rudiger, 29, ambaye anaondoka Chelsea mwishoni mwa msimu huu. ***(Goal)***

### BALOTTI AWINDWA WEST HAM

KLABU ya West Ham imejiunga katika kinyang'anyiro cha kumsaka mshambuliaji wa Torino na Italia, Andrea Belotti, 28. ***(Fichajes)***

### MBAPPE, PSG SASA SAFI

MAZUNGUMZO kati ya wawakilishi wa Kylian Mbappe, 23, na Paris St-Germain kuhusu mkataba mpya wa mshambuliaji huyo yanaendelea vema. ***(ESPN)***

### XAVI KUMBAKIZA DE JONG

KOCHA wa Barcelona, Xavi anataka kiungo wa kati, Frenkie de Jong, 24, kubaki klabuni hapo. Mholanzi huyo amehusishwa na uhamisho wa kwenda Manchester United ambao utamkutanisha tena na kocha wake wa zamani, Erik ten Hag. ***(Manchester Evening News)***

### SANGARE ATAKIWA LEICESTER

LEICESTER City inatarajia kumsajili kiungo wa kati wa PSV Eindhoven, Ibrahim Sangare, 24. Bei ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast, huenda ikawa pauni milioni 30. ***(Sun on Sunday)***

### KEANE AWINDWA WEST HAM

WEST Ham itajaribu kumsaijili, Michael Keane , 29, kutoka Everton ikiwa Toffees hao wataondolewa kwenye Ligi Kuu msimu huu. ***(Star Sunday)***

### ARSENAL KUSAJILI WAWILI

ARSENAL itazingatia kusajili mchezaji "mmoja au wawili" msimu huu wa majira ya joto, amesema mkurugenzi wa ufundi, Edu. ***(Evening Standard)***

### JUVE WAMTAKA DI MARIA

JUVENTUS imefanya mawasiliano na wawakilishi wa winga wa ParisSt-Germain, 34, Angel di Maria. ***(Gianluca di Marzio)***

### OSIMHEN EURO MIL. 80

NAPOLI wanataka angalau euro milioni 80 ikiwa wataamua kumuuza mshambuliaji wao, Victor Osimhen, 23, ambaye ni miongoni mwa walengwa wa Arsenal msimu huu wa majira ya joto. ***(CBS Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AIBEBESHA PSG UBINGWA 10 UFARANSA

**Waubeba na mechi nne mkononi, sasa wameifikia rekodi ya Saint-Etienne iliyokuwa...**

**PARIS,** Ufaransa

LIONEL Messi alifunga bao zuri wakati Paris Saint-Germain ikinyakua ubingwa wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, juzi Jumamosi baada ya kutoka sare ya 1-1 na Lens ambayo ilitoka nyuma ikimaliza na wachezaji 10 pale kwenye dimba la Parc des Princes.

PSG waliingia kwenye mchezo huo wakijua pointi moja ingetosha kutwaa taji la 10 la Ligue 1 katika historia yao na walikuwa na matumaini ya kufanya kazi hiyo wakiwa kwenye uwanja wa nyumbani.

Lens ilimpoteza Kevin Danso kwa kadi nyekundu dakika ya 57, na dakika 11 baadaye Messi akafunga bao zuri la umbali mrefu.

**Hata hivyo, muda wa kushinda taji uliharibika kwa kiasi fulani pale ulegevu wa PSG ulipomruhusu Corentin Jean kusawazisha kwa shuti kali.**

Vijana wa kocha Mauricio Pochettino walizomewa na mashabiki wa nyumbani wakati wa mapumziko, Seko Fofana na Danso wakipoteza nafasi za mapema za Lens kabla ya Achraf Hakimi na Neymar kukaribia kuifungia PSG.

PSG waliboresha kiwango chao kipindi cha pili na hatari ya Kylian Mbappe iliokolewa na Jean-Louis Leca.

Ubingwa huo umekuwa ni wa kumi wa Ligi Kuu kwa PSG katika historia yao.

PSG sasa wameifikia rekodi ya Saint-Etienne ambao ndio iliyokuwa inaongoza kwa kutwaa taji hilo mara 10.

Mataji hayo 10, nane kati yake wameshinda tangu waliponunuliwa na kampuni ya QSI mwaka 2011.

Marseille wanafuatia wakiwa wamelitwaa taji hilo mara tisa.


SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
CRYSTAL PALACE
VERSUS
LEEDS
1 | 2.03
X | 3.42
2 | 3.37

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARTETA AKUNWA MASHABIKI KUMKUBALI XHAKA



**LONDON,** England


KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, alifurahi sana kuona jinsi uhusiano wa Granit Xhaka na mashabiki ulivyoboreka baada nyota huyo kushangiliwa kwa nguvu alipofunga bao la tatu dhidi ya Manchester United, Jumamosi.

Xhaka aliifungia Arsenal bao la tatu kwenye Uwanja wa Emirates, akiachia shuti kali na kufanya mchezo kuwazidi maji 'Mashetani Wekundu' hao.

Hapo awali, United walikuwa wametishia kufutilia mbali uongozi wa Arsenal, ambao walikuwa 2-0 katika kipindi cha kwanza baada ya Cristiano Ronaldo kufunga bao na kufanya matokeo kuwa 2-1, huku Bruno Fernandez akikosa mkwaju wa penalti.

Lakini bao la Xhaka lilizima kasi ya United, na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi, alifurahishwa na shangwe alipotolewa uwajani mwishoni mwa ushindi wa mabao 3-1 wa 'Washikabunduki' hao.

Ilionesha mabadiliko makubwa ya bahati kwa Xhaka kutoka wakati alionekana kutoelewana na mashabiki, akifichua hivi majuzi kwamba karibu aondoke kwenye klabu kwa "chuki" kutoka kwa mashabiki, akidai alishapanga nguo zake kwenye mabeki Desemba 2019.



## *Lewandowski hajui hatima Bayern ikibeba ubingwa*

**MUNICH,** Ujerumani

NYOTA wa Bayern Munich, Robert Lewandowski bado hajasikia lolote kutoka kwa klabu hiyo kuhusiana na mazungumzo ya mkataba mpya, wakati timu hiyo juzi, Jumamosi ilibeba ubingwa wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga.

Lewandowski alifunga kwa mara ya 27 dhidi ya klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund, na kuipa Bayern ushindi wa mabao 3-1 na wakabeba ubingwa wa Ligi Kuu kwa msimu wa 10 mfululizo.

Hiyo ni rekodi katika ligi tano kubwa bora za Ulaya, hakuna timu iliyowahi kutwaa mataji 10 katika misimu kumi mfululizo, inafuatiwa na Juventus (mara tisa). Hata hivyo, Lewandowski anakaribia kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na Bayern, ambapo alijiunga nayo kutoka Dortmund kwa uhamisho huru mwaka 2014.

Uvumi umeongezeka kwamba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, anaweza kusonga mbele kabla ya msimu ujao, huku Barcelona wakihusishwa.

Na mshambuliaji huyo wa Poland, alithibitisha kuwa bado hajaambiwa iwapo mazungumzo kuhusu mkataba mpya yanaendelea, baada ya mchezo huo.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# YANGA VS NAMUNGO FC MECHI BORA KWANGU MSIMU HUU-KAZE

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesifu wachezaji wao kupambana na kuufanya mchezo dhidi ya Namungo FC kuwa mechi bora kwake kwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga juzi iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Namungo FC katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. Akizungumza na gazeti hili jana, Kaze alisema kwa michezo 20 ambayo tayari wameshacheza msimu huu, mechi hiyo kwake ilikuwa bora kulingana na jinsi walivyocheza na kuwazuia Namungo FC kufanya mashambulizi, lakini kutumia madhaifu yao kupata ushindi huo.

Alisema kulingana na jinsi ya wachezaji walivyojitoa na nafasi walizotengeneza kama wangezitumia vizuri wangeweza kushinda mabao matano hadi saba .

"Mchezo wa leo (juzi), wachezaji walikuja kwa dhamira ya kutafuta kitu kikubwa, hii ni baada ya kauli ya mmoja wa maofisa waliokuwa benchi la ufundi la timu nyingi (Namungo), kutupatia nguvu ya kupambana," alisema na kuongeza.

"Kauli kwamba Namungo FC anaweza kutufunga, halafu tutapoteza pointi dhidi ya Simba na kudai kwamba hatutaweza kupata ubingwa hiyo iliwatia nguvu wachezaji na kujituma zaidi katika mchezo huu," alisema Kaze.

Alisema haikuwa rahisi kwa sababu walitengeneza nafasi nyingi na kushinda kumalizia lakini pia walifanikiwa malengo yao ya kutompa nafasi mpinzani wao huyo kufanya mashambulizi.

"Tulijua mechi ya Namungo FC, tulijiandaa kulingana na mpinzani wetu, wachezaji wao wanafika katika mwili, hatukuwaruhusu na kutaka wacheze mpira, hivyo tukampeleka Bangala kucheza nyuma na kuwachezesha mbio mbio," alisema Kaze.

Alisema sasa wanaenda kujipanga kwa mchezo ujao dhidi ya Simba kuhakikisha wanafanyia kazi mapungufu yao yaliyojitokeza katika mchezo huu uliopita. Naye Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio', alisema mechi ilikuwa nzuri na wamekubali matokeo na sasa wanaenda kujipanga kwa michezo ijayo.

Alisema Yanga wamefanikiwa kuvunja mwiko wa kutopata ushindi mbele ya Namungo FC kwa misimu mitano.

Yanga sasa imecheza mechi 20 ikishinda 17, sare tatu dhidi ya Mbeya City, Simba na Namungo FC (kwenye mzunguko wa kwanza) na imejikusanya jumla ya pointi 54 ikiongoza msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 msimu huu.



Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' akijiandaa kuachia shuti, huku akizongwa na mabeki wa Namungo FC, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. Yanga ilishinda mabao 2-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Dodoma Jiji yatamba kuanza ligi

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuibamiza Mbeya City juzi usiku kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Masoud Djuma, amesema sasa ndiyo wameanza ligi na anatarajia kufanya vema kwenye mechi zingine zinazofuata.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyochezwa saa 3:00 usiku na Dodoma Jiji kushinda mabao 2-1, Djuma alisema aliwaambia wachezaji wake kuwa kama wakipoteza mechi hiyo, basi njia itakuwa ni nyeupe ya kwenda Ligi ya Championship, hivyo wakaanza kupambana kuanzia mazoezini hadi wakati wa mchezo wenyewe.

"Niliwaambia tuko pabaya, tukifungwa basi hali itakuwa mbaya zaidi tunaweza kushuka daraja, wakaanza kujituma sana kwenye mazoezi. Kwenye mechi hii tungeweza kufunga hata mabao manne kipindi cha kwanza, lakini haikuwezekana," alisema kocha huyo wa zamani wa Simba.

Hata hivyo, aliitaja sababu nyingine ni kwamba baadhi ya wachezaji wameshaanza kurejea kutoka chumba cha majeruhi hivyo kukiimarisha kikosi chake.

"Kuna baadhi ya wachezaji walikuwa majeruhi wamerejea, hasa kwenye eneo la beki wa kati, unapokuwa huna beki wa kati mrefu kwenye timu, mara nyingi inakuwa ni matatizo tu, hivyo sasa mabeki wamepona, na baadhi ya watu wameanza kutusapoti, unajua wakati wa matatizo ndipo utajua ndugu wa kweli, ndiyo kwanza sasa kazi imeanza, ndiyo tumeanza ligi," alisema kocha huyo.

Dodoma Jiji imekwea hadi nafasi ya 10, ikiwa imefikisha pointi 24 wakati Mbeya City ikiwa nafasi ya saba na pointi zake 25.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMATATU - 25/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1409 | Tuzlaspor vs Adanaspor | 2.41 | 2.97 | 2.87 |
| 15:00 | 1939 | Barnsley U23 vs Bristol City U23 | 3.45 | 4.18 | 1.75 |
| 15:00 | 2206 | Crewe U23 vs Charlton U23 | 3.80 | 3.90 | 1.72 |
| 16:00 | 5138 | Crotone vs Cremonese | 4.54 | 3.56 | 1.73 |
| 17:00 | 3345 | Swansea U23 vs Colchester U23 | 1.77 | 3.74 | 3.74 |
| 17:30 | 4004 | CD Trofense vs Varzim | 2.44 | 3.20 | 2.76 |
| 18:00 | 1613 | Sassuolo Youth vs Empoli Youth | 2.02 | 3.55 | 3.40 |
| 18:00 | 1662 | Honka vs Seinajoen JK | 2.22 | 3.01 | 3.16 |
| 18:00 | 3572 | Argesul Pitesti vs Universitatea Craiova | 4.46 | 3.32 | 1.80 |
| 18:00 | 5095 | Pyunik Yerevan vs FC Noravank | 1.46 | 4.10 | 7.20 |
| 18:30 | 4376 | NK Aluminij vs NK Celje | 3.25 | 3.25 | 2.07 |
| 18:30 | 5180 | PK-35 vs Pif Jalkapallo | 1.42 | 4.27 | 6.22 |
| 19:00 | 1018 | Stabaek vs Sandnes Ulf | 1.64 | 3.90 | 4.29 |
| 19:00 | 1688 | Benevento vs Ternana | 1.55 | 4.06 | 5.35 |
| 19:00 | 2708 | Como vs Vicenza | 3.07 | 3.32 | 2.21 |
| 19:00 | 2820 | Mjondalen vs Fredrikstad | 2.04 | 3.49 | 3.10 |
| 19:00 | 5331 | FC Krasnodar vs Zenit St Petersburg | 6.75 | 4.96 | 1.37 |
| 19:00 | 5613 | Brescia vs Spal | 1.59 | 3.76 | 5.35 |
| 20:00 | 1372 | Viktoria Koln vs Meppen | 1.72 | 3.66 | 4.45 |
| 20:00 | 1643 | Sporting Braga vs Porto | 3.98 | 3.68 | 1.81 |
| 20:00 | 2121 | IFK Varnamo vs Degerfors | 2.15 | 3.30 | 3.01 |
| 20:00 | 2883 | Brondby vs Midtjylland | 3.14 | 3.39 | 2.17 |
| 20:00 | 3301 | Wisla Krakow vs Wisla Plock | 1.86 | 3.40 | 3.74 |
| 20:00 | 3524 | Elfsborg vs GIF Sundsvall | 1.35 | 4.67 | 6.81 |
| 20:00 | 4007 | Osters IF vs Vasteras SK | 1.87 | 3.50 | 4.16 |
| 20:00 | 5018 | Landskrona Bois vs Orgryte IS | 3.03 | 3.29 | 2.35 |
| 20:00 | 5192 | Sirius FK vs Hammarby | 4.37 | 3.88 | 1.63 |
| 20:10 | 4740 | Malmo vs IFK Goteborg | 1.45 | 4.07 | 6.01 |
| 20:30 | 1859 | Samsunspor vs Altinordu | 1.49 | 3.99 | 5.64 |
| 20:30 | 2552 | Besiktas vs Kasimpasa | 1.75 | 3.82 | 4.16 |
| 20:30 | 2787 | Sivasspor vs Alanyaspor | 2.25 | 3.28 | 3.08 |
| 21:00 | 2093 | Brighton U23 vs Chelsea U23 | 2.29 | 4.27 | 2.33 |
| 21:00 | 3000 | Blackburn Rovers U23 vs Crystal Palace U23 | 2.21 | 3.75 | 2.63 |
| 21:00 | 3455 | Jong Ajax vs VVV Venlo | 1.56 | 4.45 | 4.55 |
| 21:00 | 3732 | Hafnarfjordur vs Fram Reykjavik | 1.37 | 4.67 | 6.41 |
| 21:00 | 4406 | Derby County U23 vs Tottenham U23 | 2.68 | 3.80 | 2.15 |
| 21:00 | 4420 | Leicester U23 vs Liverpool U23 | 2.82 | 4.28 | 1.95 |
| 21:00 | 4732 | Everton U23 vs West Ham U23 | 2.77 | 4.37 | 1.96 |
| 21:00 | 5236 | Jong PSV vs Maastricht | 1.39 | 4.83 | 6.31 |
| 21:00 | 5570 | KR Reykjavik vs Breidablik | 2.53 | 3.41 | 2.43 |
| 21:30 | 3084 | Preston vs Blackburn | 2.63 | 3.07 | 2.68 |
| 21:30 | 3436 | Perugia vs Parma | 1.96 | 3.26 | 3.81 |
| 21:45 | 2742 | Sassuolo vs Juventus | 3.90 | 3.66 | 1.82 |
| 21:45 | 4270 | Toulouse vs Niort | 1.34 | 4.76 | 8.13 |
| 22:00 | 2062 | Crystal Palace vs Leeds | 2.03 | 3.42 | 3.37 |
| 22:00 | 5456 | Almeria vs Sporting Gijon | 1.57 | 3.82 | 5.55 |
| 22:30 | 1028 | Smouha Club vs Misr Lel Makasa | 1.80 | 3.18 | 4.87 |
| 22:30 | 2225 | Coca Cola vs El Gouna | 1.58 | 3.74 | 5.78 |
| 22:30 | 4591 | Boavista vs Sporting Lisbon | 7.17 | 4.28 | 1.42 |
| 22:30 | 5863 | Ghazl EL Mahallah vs Farco FC | 2.68 | 2.73 | 2.98 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatatu Aprili 24, 2022

Nipashe



Messi aibebesha PSG ubingwa 10

UKURASA 21

WANGU HUU...



Beki wa Simba, Shomari Kapombe (kushoto), akiwania kumiliki mpira dhidi ya mshambuliaji wa Orlando Pirates Deon Hotto, kwenye mechi ya robo fainali mkondo wa pili ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Orlando, Soweto, Afrika Kusini na kumalizaka kwa wenyeji kushinda kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 4-3 baada ya kushinda 1-0, hivyo matokeo ya jumla kuwa 1-1. **PICHA: SIMBA**

## Yanga Princess 'yaionja' Simba Queens pungufu

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara ya kwanza kwenye historia ya timu za mpira wa miguu wa wanawake, timu ya soka ya Yanga Queens imepata ushindi kwa kuwafunga watani zao wa jadi, Simba Queens bao 1-0 jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dara Salaam.

Lilikuwa ni bao la dakika ya 45 lililowekwa wavuni na Clara Luvanda, aliyepiga shuti ambalo lilidakwa na kipa Gelwa Yona, lakini ulimponyoka na kujaa wavuni.

Hii ni mara ya kwanza kwa Simba Queens kupoteza mechi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, baada ya kushinda mechi zote 14, kabla ya kukubali kipigo hicho jana

Simba Queens ilipata pigo dakika ya tano tu ya mchezo baada ya beki wake wa kati Juliet Singano kutwangwa kadi nyekundu, alipoinua mguu juu na kumgusa kichani mchezaji wa Yanga Princess, Lucia Mrema.

Kutolewa mapema kwa mchezaji huyo kulionekana kuwachanganya wachezaji wa Simba Queens na kuwapa nafasi Yanga Princess kuutawala mchezo kwa asilimia kubwa kipindi chote cha kwanza.

Luvanda ndiye alionekana mwiba mchungu kwa mabeki wa Simba Queens na angeweza kuipatia timu yake mabao mawili zaidi kama angetulia. Angalau kipindi cha pili baada ya kufanya mabadiliko kadhaa Simba Queen ilionekana kutulia, lakini tatizo kubwa lilikuwa wachezaji wake kuonekana kukosa nguvu kuliko wenzao.

Pamoja na kupoteza, Simba Queens inaendelea kuongoza ligi ikiwa na pointi 42, huku Yanga Princess ikiendelea kuwa kwenye nafasi ya tatu kwa pointi 35.

# Simba yatolewa kishujaa

**Na Adam Fungamwango**

## Yafia kwenye matuta baada ya kucheza dakika 34 pungufu, penalti za Inonga, Mkude zaiua...

SAFARI ya wawakilishi wa Tanzania kwenye Kombe la Shiriksho la Soka Afrika, Simba imemalizika jana kwenye hatua ya robo fainali, baada ya kutolewa kwa mikwaju ya penalti 4-3 kwenye mechi ya mkondo wa pili iliyopigwa Uwanja wa Orlando, mjini Soweto dhidi ya Orlando Pirates.

**Timu hizo zililazimika kupigiana mikwaju ya penalti baada ya Simba kufungwa bao 1-0 kwenye mechi ya jana, huku ikiwa imeshinda 1-0 wiki moja iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, hivyo matokeo ya jumla kuwa sare ya bao 1-1.**

Jonas Mkude na Enock Inonga ndiyo waliwafanya mashabiki wa Simba watoke vichwa chini baada kukosa penalti zao, huku Shomari Kapombe, Mohamed Hussein na Meddie Kagere wakizamisha zao kimyani.

Penalti za wenyeji zilitumbulizwa wavuni na Deon Hotto, Gabadinho Mhango, Abel Mabaso, na kipa Richard Offori, huku Aishi Manula akipangua penalti ya Kabelo Dlamini.

Mechi ilianza kwa Simba kufika langoni mwa wenyeji wao kwa shambulizi dhaifu, lakini dakika ya pili tu Orlando Pirates walijibu kwa shambulio kali, Kwame Peprah akipata nafasi nzuri baada ya Manula kutema kombora kali la Diotto, lakini akapaisha mpira juu.

Diotto aliyeonekana kuwa ndiye mpiga faulo wa kutegemewa wa Orlando Pitates, nusura aipatie timu yake bao dakika ya nne ya mchezo, kwa kutandika shuti kali kwa mpira wa kutengwa, lakini Manula alichupa na kupangua.

Mfululizo na mashambulizi uliendelea kwenye lango la Simba, kwani pasi maridadi ya Bandile Shandu ilimkuta Landu akiwa kwenye nafasi nzuri, akaachia 'mashine' iliyokwenda moja kwa moja mikononi mwa Manula.

Kipa huyo namba moja Tanzania, aligongana na Kwame katika harakati za kuokoa na kuumia dakika ya 16. Kwa mara nyingine tena, Manula aliiokoa Simba kuzama dakika ya 45, alipodaka kwa ustadi shuti la Shandu.

Dakika ya 56 kipindi cha pili, Simba ililazimika kucheza pungufu baada ya straika wake, Chris Mugalu kuonyeshwa kadi nyekundu, ikiwa ni ya pili ya njano, baada ya kumchezea vibaya beki Innocent Maela.

Ilikuwa kama mkosi, kwani dakika tatu baadaye, Kwame aliipatia timu yake bao kwa kichwa, baada ya mabeki wa Simba kushindwa kucheza krosi iliyopigwa na Ntsekeleli Nyauza.

Kwa matokeo hayo, Orlando Pirates sasa itavaana na mshindi wa mechi ya jana usiku kati ya Al Ahli Tripoli na Al-Ittihad zote za Libya.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >